Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Tatu – Tarehe 10 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMARY YUSSUF MZEE):**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2009 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011.

Taarifa ya Sera na Fedha kwa Kipindi cha Mwaka 2009/2010 na Mwelekeo wa Sera za Fedha kwa Mwaka 2010/2011.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi, namwita sasa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Baada ya Serikali kuubinafsisha Mradi wa Kiwira hatimaye imeuchukua Mradi huo na sasa hivi unapoteza si chini ya shilingi bilioni tano kwa mwaka kwa sababu hakuna kinachozalishwa; ni nini msimamo wa Serikali juu ya Mradi huo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Hamad, swali lake zuri sana kama ifuatavyo:-

Mimi sina takwimu hasa kwa hili analolisema lakini inawezekana pengine lina ukweli. Kampuni hii hii ambayo ilifika mahali ikashindwa hata kulipa mishahara, kama wamefikia kiwango hicho kwa sababu tu imesimama, basi nadhani changamoto ni ya Serikali lakini tulikwishakulieleza jambo hili kuwa baada ya uamuzi wa Serikali wa kuchukua zile hisa, sasa taratibu zinaendelea kukamilishwa kwa maana ya kupata mtaalam atakayefanya tathmini ya zile hisa tuweze kujua thamani yake, tuondoe mzigo wa Serikali ambao tumeubeba, kile kitakachobaki tukubaliane namna ya kukilipa, tukishamaliza hilo tutaendelea.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa kuchelewa kutoa maamuzi kwa Serikali kunasababisha mitambo iliyoko pale kuchakaa na Wafanyakazi wanalipwa fedha ambayo hawaizalishii; huoni kwamba Serikali inabeba mzigo usio wa lazima wakati wawekezaji wamekuja na tumewapeleka mpaka kwa Waziri na kwamba wako tayari kuuendesha Mradi ule na kuongeza megawati 200 za umeme lakini Serikali imeshindwa kutoa maamuzi. Je, huoni kuchelewa kwa Serikali kutoa maamuzi kutaendelea kutubebesha Watanzania mzigo usio na sababu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hakuna anayeweza kufanya jambo zima ambalo limekuja la neema kama hilo na baadaye kwa makusudi tu ukaamua kulipuuza, hayupo mtu wa namna hiyo. Tunachosema hapa ni kwamba, tunachojaribu kufanya ni kuzingatia taratibu zetu za nchi ili tuweze kuwa na mradi ambao tunajua hautatuletea maneno mbele ya safari, tukishamaliza hili na mimi ninaamini kwa kasi tunayokwenda nayo, hatutachukua muda mrefu kabla hatujalimaliza.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kufikia makubaliano na kutiwa sahihi zile kero za Muungano, siku ya tarehe mbili mwezi wa sita (2 Juni, 2010).

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ikiwa katika kipindi cha miaka 46 ni mambo mawili tu ambayo mmekubaliana na yametiwa sahihi hivi juzi. Je, ni mangapi yaliyobakia kama kero za Muungano na lini yatafanyiwa ufumbuzi ili kukamilika?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Mnyaa, swali lake kama ifutavyo:-

Kwanza ni vizuri tukajua historia kidogo ya tatizo hili. Masuala haya yanayoleta kero kati ya Serikali hizi mbili, yalifanyiwa kazi na Kamati ya Mzee Shellukindo, tangu mwaka 1992 na katika kazi ile yalikuwepo masuala 31 ambayo yalitakiwa yazungumzwe na tuone kama tunaweza tukaafikiana. Mengine yalihusu mabadiliko au kufanyika kwa mabadiliko katika Katiba zetu mbili. Mengine yalitakiwa yatungiwe Sheria na yako mengine ambayo ilibidi tu kwa kutumia taratibu za kiutawala kufanya maamuzi ya kisera.

Mheshimiwa Spika, katika masuala 31 haya, mengi sana yamekwishafanyika. Tayari Katiba zimebadilishwa na Sheria zimebadilishwa katika kukidhi mahitaji ya hiki tunachokiita kero za Muungano. Hiki tulichokifanya juzi ni katika baadhi ya maeneo

machache yaliyokuwa yamebaki, tukaona kama utaratibu wa kawaida ulivyo, nayo tuyakamilishe kwa njia hiyo. Kama kuna mambo makubwa yamebaki, pengine siyo mengi sana na sidhani kama yatachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi niseme tu kwamba, masuala ya Muungano haya ni makubwa na yana mambo mengi ambayo muda wote lazima muendelee kuleana na kujaribu katika mtazamo ambao utafika mahali uwezeshe watu waweze kuishi kwa amani.

Mimi siamini kwamba, hata baada ya kumaliza masuala mawili, matatu, manne yaliyobaki, kero za Muungano zitakuwa zimekwisha kwa sababu yataibuka mambo mengine na mtaendelea kuyazungumza kadiri yanavyoibuka ili muendelee kuuimarisha Muungano huo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Canada mpaka leo bado hawajafikia muafaka. Ireland na Uingereza mpaka leo hawajafikia muafaka, lakini Muungano upo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ndiyo maana ninasema kilichobaki si kikubwa kama tulikotoka. *(Makofi)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu yenye mwelekeo mzuri lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hizi kero kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu zilikuwa 31; ziko pia nyingine ndogo ndogo na kero kuu bado kama nane mpaka kumi ambazo zinahusiana na *TRA, BoT,* Mkopo wa Nje, Uvuvi wa Bahari Kuu na Mgawanyo wa Mapato. Sasa suala hili limekuwa pana na hasa katika shughuli ya Katiba ilivyo hivi sasa ambapo mkanganyiko mkubwa wa hizi kero ni kutokana na Katiba.

Je, huoni sasa wakati umefika wa hii Katiba kubadilishwa ikapatikana Katiba mpya ambayo itahusiana mchango wa Watanzania wote walio na vyama na wasio na vyama?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nilijua Mheshimiwa Mnyaa atapandia hapo hapo, lakini sidhani kwa kweli kama utakuwa unanitendea haki. Kikubwa hapo unachokisema ni kwamba, kwa kero zilizobaki Serikali imejipangaje kuzimaliza. Jibu langu hapa tena ni rahisi tu ni kwamba, zipo kero ambazo haziwezi kutatuliwa kwa mfumo wa mazungumzo kwa kutumia Kamati ya Makamu wa Rais, ndiyo maana katika mapendekezo ya Mzee Shellukindo, lilikuwepo pendekezo mahususi la Tume ya Pamoja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu yapo masuala pale kama unayosema ya kifedha, ya benki, madeni na masuala mengine ya mikopo, ambayo kwa ushauri mzuri wa Kamati ya Mzee Shellukindo, Tume hiyo ndiyo inatakiwa sasa iyazamie kwa utaratibu wa kawaida na kuweka utaratibu ambao utatuwezesha kwenda mbele zaidi. Sasa hili ukilitumbukiza tu kwamba hapo ndiyo mahali pake pa kufanya mabadiliko kuandika

Katiba mpya, sidhani kama ni mahali pake. Ninadhani kama una *agenda* hiyo ije tofauti tuizungumze tofauti, lakini tusichanganye na hili jambo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, huu ni Mwaka wa Uchaguzi na tunategemea kwamba Uchaguzi huu hautavurugwa kwa njia yoyote ile. Hivi karibuni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wametangaza kwamba Vyuo vya Elimu ya Juu watafungua mwezi Novemba, 2010 badala ya Oktoba kama ilivyo kawaida kutokana na uchelewaji wa usajili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza.

Huoni kwamba kwa tamko hilo wale wanafunzi wanaoendelea ambao ni wengi sana walishajiandikisha katika vyuo vyao wakijua kwamba vyuo vinafunguliwa Octoba; watakosa haki yao ya msingi ya kupiga kura? Je, Serikali ina mkakati gani sasa kuhakikisha kwamba vijana hawa watapiga kura?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, suala analoliuliza dada yangu Susan Lyimo kusema kweli si la wanafunzi tu, litahusu Watanzania wengi, ambao wakati wa uchaguzi hawatakuwa katika maeneo ambayo walikuwa wamejiandikisha.

Kwa hiyo, Tume ilichofanya itaweka utaratibu muda mfupi ujao, kuwapa muda wa kutosha wale wote ambao watakuwa katika maeneo tofauti na walikojiandikisha, waweze kuchukua hatua za kufanya marekebisho kwa kujiandikisha maeneo hayo ili takwimu zile ziweze kuhamishwa na kupelekwa katika vituo vyao vipya watakakopigia kura. Kwa hiyo, hilo nadhani litasaidia sana kuondoa hofu iliyoko kwa Watanzania wote kwa ujumla na siyo kwa wanafunzi tu peke yao.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni katika Kijiji cha Kebweye, Kata ya Nyakonga, akina mama walitendewa matendo ambayo ni ya aibu na Jeshi la Polisi ambapo Askari wa Jeshi la Polisi waliamuru akina mama wawavue suruali na chupi halafu wakaamuru kwamba wawalambe na kuwanyonya sehemu za siri.

Je, Serikali ina tamko gani kuhusu aibu hii?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, pengine kama Serikali, tuanze kwa kusema kama kweli yametokea haya kwanza tunawaomba radhi Watanzania, kwa sababu si jambo ambalo ungelitegemea katika jamii yetu kwamba tungeweza kuwa na chombo ambacho kinaweza kufanya udhalimu wa namna hiyo. Ninasema kama ni kweli, lakini maadam umeuliza Mheshimiwa Mwera, nataka nikuahidi baada tu ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu hapa, nitakuomba tukutane pamoja na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ambaye yuko hapa au Waziri mwenyewe, tupate maelezo kidogo ya undani ili tuweze kulifanyia kazi haraka sana suala hili kwa sababu ni kitendo cha kinyama, cha ovyo na wala si utendaji mzuri wa chombo hata kidogo.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:**Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**SPIKA:** Waheshimiwa, naomba utulivu tusikilize swali linalofuata.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kanisa Katoliki liliomba kujenga au kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Kangwa iliyoko Mjini Musoma na hospitali ile ilijengwa kwa nguvu za Wananchi kwa kuchanga fedha zao, kwa kuuza mali zao na hatimaye wakaweza kufika mahala wakahitaji nguvu ya Serikali.

Pamoja na Kanisa Katoliki kukubali nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu Mstaafu, alikuja pale akaamua kuwakabidhi kama walivyokuwa wameomba na Serikali ikaahidi kuwa ingeweza kuwakabidhi Hati, yaani kumkabidhi Baba Askofu pamoja na kulipa fidia ambayo ilikuwa takriban kama shilingi milioni 35.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, cha kusikitisha ni kwamba, zoezi la kulipa fidia hiyo ...

**SPIKA:** Nenda kwenye swali Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Zoezi hilo limechukua muda mrefu na nilikuja hapa Bungeni nikauliza swali mwezi wa 11 na Serikali ikaahidi kwamba, ingelipa fidia hiyo mara moja lakini matokeo yake fidia haikulipwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa, nitakuzuia nasema uliza swali.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, swali. Baada ya Baba Askofu kuamua kutoiendeleza Hospitali hiyo, baada ya kuwa fidia kutolipwa. Je, Serikali sasa ipo tayari kwa mwaka huu wa fedha kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi huo kutokana na nguvu nyingi za Wananchi kupotea pasipo Serikalli kutimiza wajibu wake? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu ndugu yangu, Mheshimiwa Mnyinyi, swali lake kama ifuatavyo.

Mimi naona kuna tatizo mahali fulani. Kama unachozungumza ni shilingi milioni 35 na umeuliza hapa Bungeni wakakwambia zitalipwa na nilikuwa karibu nikuulize baada ya pale ulifanya nini? Ulikaa tu ama ulichukua hatua za kwenda Wizarani pale kwa sababu nina hakika kama kungekuwa na ufuatiliaji wa karibu, sidhani kama ingechukua muda mrefu kiasi hiki.

Sasa tupo kwenye dakika za lala salama hizi, nashindwa hata kusema nisaidie nini, lakini Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, yuko hapa na Waziri wa Fedha yupo, niwaombe tu jamani milioni 35 si pesa nyingi za kufanya Serikali iulizwe swali hapa

Bungeni. Hebu limalizeni haraka ili Watanzania hawa waweze kuendelea na kazi zao. *(Makofi)*

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama nilivyosema; baada ya fedha hizo kutolipwa Baba Askofu ameamua kutoendelea na ujenzi huo; ndiyo maana ninasema kwa kuwa nguvu za Wananchi zimeingia pale. Je, Serikali ipo tayari kuanza kujenga hospitali hiyo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nami nasema tusianze kuzua kesi mpya. Mheshimiwa Manyinyi, nina hakika mkikaa na Baba Askofu mkazungumza, hawa Viongozi wa Madhehebu ya Dini, hawana hasira kama tulizonazo wengine. Ataelewa na nina hakika ataendelea na Mradi huo wa ujenzi, alishaukubali ni vizuri akauendeleza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu yamekwisha. Kwa mara nyingine tena, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Katibu kwa shughuli inayofuata.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 21

### Kudhibiti Migomo/Maandamano Nchini

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA (K.n.y. MHE. MAULIDAH ANNA KOMU** aliuliza:-

Kwa kuwa migomo, maandamano imekuwa ni jambo la kawaida katika nchi yetu hususani Jijini Dar es Salaam na kwamba hali hiyo husababishwa na madai ya muda mrefu kwa kundi husika:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kuhakikisha madai yote ya vikundi yanatiliwa maanani na kutekelezwa kwa wakati muafaka bila ucheleweshwaji?

(b)Je, Serikali haioni kwamba kwa kuacha Migomo/maadamano hayo kuendelea ni kusababisha vurugu na uvunjaji wa amani hasa pale mabomu ya machozi na maji ya kuwasha vinapotumika?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali hili naomba nimpongeze Waziri Mkuu kwa kujibu maswali ya papo kwa papo kwa umahiri mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulida Anna Komu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kusema kuwa migomo na maandamano halali inayozingatia sheria za nchi na pia mazingira ya hali halisi ya eneo na wakati ni sehemu ya haki za msingi za binadamu na raia ambazo zimeainishwa katika Katiba ya nchi yetu. Sheria na Kanuni zinazosimamia masuala yanayohusu madai ya haki ya kundi/makundi ya watu katika jamii dhidi ya Serikali au taasisi binafsi ni pamoja na sheria ya ajira na mahusiano kazini sheria Na. 6 ya mwaka 2004 (*The Employment and Labour Relations Act, No. 6 of* 2004), sheria ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2002 *(The Police Auxiliary Service Act,2002)* na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2002 (*The Political Parties Act*, 2002). Sheria hizi zinaanisha taratibu za kuzingatiwa katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa madai yanayolalamikiwa pamoja na hatua za kuchukua endapo taratibu zimekiukwa.

Katika taratibu hizo migomo au maandamano imeainishwa kama hatua ya mwisho ya kushinikiza utekelezwaji wa madai husika. Katika kipindi cha mwaka uliopita kwa nyakati tofauti tulishuhudia baadhi ya makundi katika jamii yetu yakitekeleza hatua hiyo ya migomo na maandamano bila kuzingatia matakwa ya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, ni vema wananchi wafahamu kwamba jukumu la Serikali yeyote ya kidemokrasia kama ilivyo Serikali yetu, ni kusimamia rasilimali na ustawi wa nchi na wananchi wake bila ubaguzi wa aina yeyote.

Aidha ni wajibu wa wananchi kuhakikisha kwamba wanazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo ikiwa ni pamoja na kupokea na kutii maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Serikali kuhusu masuala yote muhimu ya kijamii, kwani duniani kote hakuna haki isiyokuwa na wajibu.

Mheshimiwa Spika, migomo na maandamano yanayosababisha vyombo vyetu vya dola kutumia mabomu ya machozi na maji yanayowasha huwa ni hatua ya mwisho ya kuhakikisha kwamba amani inadumishwa na haki ya wananchi wote inaendelea kuhifadhiwa kwa maslahi ya wote. Ni utaratibu unaofahamika kisheria kwamba kabla ya utekelezwaji wa hatua hii tahadhari hutolewa kwa wahusika kuacha vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na amri ya kutawanyika na kuondoka eneo la tukio mapema iwezekanavyo. Wale wanaokaidi amri hiyo huondolewa kwa nguvu.

Napenda kutumia fursa hii kuwaasa Watanzania wenzangu wote kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na mazungumzo ya pamoja katika kufikisha madai yao, kwani Serikali inao viongozi wasikivu na wenye hekima na busara kuweza kupokea na kutafakari vyema madai yao.

Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba malalamiko na madai mbalimbali yaliyowasilishwa na kuhakikiwa yatakuwa yamelipwa yote ifikapo tarehe 30 Juni, 2010.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Waziri amejielekeza sana kwenye masuala la madai ya Wafanyakazi, lakini maswali mawili ya msingi ni mapana kuliko hapo.

Je, kwa kuwa maandamano ni njia mojawapo ambayo wananchi au makundi duniani kote yanatumia nafasi hiyo kufikisha hisia zao na mawazo yao kwa Serikali yao.

(a)Je, katika swali (b) ambalo Waziri hakulijibu Serikali inaamini kwamba migomo hiyo na maandamano hayo ambayo ni ya amani na ukishataja ni ya amani, maana yake ni ya amani isipokuwa pale ambapo Polisi wanaenda kusukuma wananchi ndiyo maana wananchi wanajibu kwa vurugu. Je, Serikali inaamini kwamba maandamano ya amani yanavurugwa kweli amani ya nchi kiasi kwamba Polisi waingie kwa kutumia mabavu na kwa nini Serikali inawazuia?

(b)Je, ni kwa nini maandamano ya amani yanapopangwa na wananchi wanaeleza kwamba wanania ya kufanya maandamano kweli ya amani ni kwa nini kila wakati Polisi inatumia visingizio vya kutokuwa na polisi wa kutosha wakati ni dhahiri kabisa Polisi wanaonekana wapo kwenye maeneo hayo lakini hawapo eti kwa sababu tu ya kulinda amani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, katika kujibu swali la msingi nilitaja mambo muhimu mawili, kwamba wananchi wanawajibu wa kutii sheria, lakini pia hakuna haki ambayo haina mipaka.

Mheshimiwa Mbunge, ameapa kwa kutumia Katiba ya Nchi, Katiba ya nchi yetu hasa ile sehemu ya Haki za Binadamu inaeleza wazi kwa kuweka haki lakini papo hapo inaweka na majukumu, hii ndiyo Katiba ilivyo.

Mheshimiwa Spika, busara hii ya Katiba inalenga kwa wale ambao wanaandamana wasiingilie haki za wale raia wengine ambao hawaandamani kwa wao wenyewe lakini pia kwa mali zao. Mwenye duka barabara ya Uhuru au Msimbazi asije akafunga biashara yake kwa ajili ya maandamano au mali yake ikaharibiwa kwa kusababishwa na maandamano.

Hiyo ndiyo ndiyo dhana nzima ya haki ambayo haina mipaka, lazima isimamiwe kwa kutumia sheria na ndivyo Katiba yetu ilivyo na Katiba za nchi zote duniani ambazo zinathamini uhuru na mipaka ya haki za binadamu.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali mara nyingi imekuwa inakimbilia mahakamani kupinga maandamano pale ambapo wafanyakazi wanataka kuonesha hisia zao kwa Serikali. Serikali haitambui kwamba kuzuia maandamano halali ni kusababisha migomo baridi ndani ya sehemu za wafanyakazi suala ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri sana huduma na hasa wanaoathirika zaidi ni wananchi wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyoeleza katika majibu ya swali la msingi kwamba maandamano na migomo ni haki ya kikatiba, lakini haki hii ina mipaka yake kwa sababu sheria inalinda wananchi wote wa Tanzania.

Maandamano yanapofanyika pale Dar es Salaam kwa mfano, watu wengi namna ile katika mitaa hutarajii kwamba yataishia kwa amani, na ndiyo maana Serikali wakati mwingine kwa kutumia sheria zetu huenda mahakamani kuzuia maandamano kama hayo.

Suala la migomo baridi Serikali haina habari nayo nadhani kama kuna jambo kama hilo basi wahusika itabidi wawachukulie hatua za kisheria wanaofanya hivyo.

Na. 22

**Sera ya Utawala Bora Nchini**

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS** aliuliza:

Kwa kuwa, Tanzania inafuata sera ya utawala Bora na wananchi wake wanafurahishwa na kuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, kwa kuwasimamisha kazi viongozi waliokiuka maadili ya kazi.

Je, kwa nini zoezi hilo lisiendelezwe nchi nzima ambako kuna kasoro kama hizo zilizojitokeza huko Bagamoyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uendeshaji wa Serikali ya Kidemokrasia mara zote huzingatia utawala wa sheria (Utawala Bora) katika kufanya maamuzi yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuzingatia Utawala wa Sheria aliamua kuwasimamisha kazi baadhi ya watendaji wakuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo baada ya kupokea tuhuma mbalimbali. Baada ya kuwasimamisha kazi aliteua timu ya kufanya uchunguzi wa kina wakati watendaji wakuu hao wakiwaa wamesimamishwa kazi kuruhusu uchunguzi huru kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ili kubaini kasoro mbalimbali za uendeshaji wa Halmashauri nchini, Waziri Mkuu ameagiza kufanyika uchunguzi katika baadhi ya Halmashauri zilizotuhumiwa kwa ubadhirifu wa fedha za umma. Hadi sasa uchunguzi huu unaendelea katika sehemu mbalimbali za nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua mbalimbali za kinidhamu zinatarajiwa kuchukuliwa dhidi ya watumishi wote waliobainika na watakaobainika kufanya ubadhirifu huo kwa kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za fedha. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kufukuzwa kazi, kupunguziwa madaraka na wengine kuonywa kutegemeana na aina ya kosa.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa onyo kwa mamlaka za Serikali ambazo zimeendelea kutumia vibaya fedha za umma kuwa, kuanzia sasa mtumishi yeyote atakayebainika kufuja fedha za umma, hatua za kinidhamu zitachukuliwa mara moja na bila kuonewa huruma kwa mujibu wa sheria zilizopo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa uamuzi wa kuwasimamisha kazi baadhi ya watendaji wakuu wa Halmashauri ya Bagamoyo ulifanywa na kiongozi wa ngazi ya juu ya kitaifa, baadhi ya Watanzania wana mashaka kwamba taratibu za kiutumishi hazikufuatwa.

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu mashtaka haya ya Tanzania?

(b) Kwa kuwa tatizo la Bagamoyo limeenea katika Halmashauri nyingi hapa Nchini kama inavyojitokeza katika ripoti ya *CAG*. Je kwa nini Bagamoyo imekuwa ni mfano wa kwanza na pekee katika Serikali ya awamu ya nne ambayo iko ukingoni sasa hivi, wakati kuna Halmashauri nyingi ambazo zina matatizo kama hayo, kuna nini Bagamoyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa ana wasiwasi kwamba hatua za kiutumishi hazikufuatwa kwa kuwa wale waliosimamishwa wamesimamishwa na Waziri Mkuu. Kwanza napenda afahamu kwamba Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ni Waziri Mkuu. Kwa hiyo, alikuwa sahihi kuwasimamisha ili uchunguzi ufanyike na hatua za kinidhamu ziweze kufuata.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwanini Bagamoyo. Katika jibu langu la Msingi nimesema kwamba uchunguzi unaendelea katika Halmashauri mbalimbali, lakini Halmashauri ya Bagamoyo ilikuwa ya kwanza katika kukamilisha uchunguzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Halmashauri zingine ambazo uchunguzi unaendelea na nyingine zinakaribia kumalizika ambazo baadhi yao ni Halmashauri ya Wilaya za

Rombo, Kilosa, Ngorongoro, Arusha, Mwanga, Ileje, Karagwe na Bagamoyo ambayo tayari nimeshaitolea ufafanuzi. (*Makofi*)

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale ambao watabainika au waliobainika kukiuka maadili ya kiutumishi.

Kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2007 ilibainika Halmashauri 28 hazikurudisha fedha Hazina shilingi milioni mia nne themanini na mbili, kinyume na sheria za fedha, kifungu cha 115(3). Kwa kuwa mpaka leo hakuna hatua ambazo zimechukuliwa za dhahiri kabisa.

Je, kwanini basi mpaka leo watu hawa wanaachiwa wanadunda dunda tu ndani ya Halmashauri za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bila kuchukuliwa hatua?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kutokurudisha fedha Hazina haina maana kwamba kuna wizi umetendeka.

Kwa hiyo, *CAG* anapohoji kama maelezo yametolewa na sababu za kutokurejesha fedha zinaeleweka hakuna sababu yeyote ya kuzichukulia hatua Halmashauri hizo. Unaweza ukakuta labda hizo pesa zilikuwa tayari kwenye miradi, kuna Wakandarasi ambao walikuwa wanafanya kazi ambao walihitajika walipwe hizo pesa. Kwa hiyo, kama hao watumishi hawakuchukuliwa hatua nadhani kuna sababu za msingi. Si kila hoja inayohojiwa inatakiwa mtu achukuliwe hatua. (*Makofi*)

Na. 23

**Fedha za Ukimwi Kupelekwa kwa Waathirika**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa UKIMWI ni janga linaloendelea kupoteza vijana wengi ambao ndio nguvu kazi ya taifa na kwa kuwa Serikali inajitahidi kutoa fedha nyingi kwa ajili ya semina, Makongamano, Vipeperushi na matangazo mbalimbali katika vyombo vya habari kwa lengo la kuwaelimisha wananchi wote juu ya ugonjwa huo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka fedha hizo sasa kwa waathirika wenyewe ili wapatiwe elimu na lishe bora ili kuwapunguzia ukali wa maisha?

**SPIKA**: Kabla sijamwita Waziri wa Afya kujibu swali, mtaona leo katika maswali baada ya maswali ya Waziri Mkuu yote yamepangwa ni ya Kambi ya Upinzani. Hii siyo hali ya kawaida, wala haikubaliki kwa sababu Bunge hili ni la Vyama vingi. Kwa hiyo, namwelekeza Katibu achunguze hawa Wapinzani ni wajanja sana, inawezekana kabisa kuna mbinu fulani imetumika. Haiwezekani maswali asilimia mia

moja yakatoka Kambi ya Upinzani. Kwa hiyo, namwagiza Katibu awe mwangalifu hali hii isijitokeze tena. (*Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la ugonjwa wa UKIMWI hapa nchini, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na wadau wengine, wanatekeleza afua (*interventions*) mbali mbali ambazo zimethibitishwa kuwa zinatoa tija katika udhibiti wa ugonjwa wa UKIMWI *(evidence based).*

Afua hizo ni pamoja na elimu yenye lengo la kuleta mabadiliko ya tabia, usambazaji wa mipira ya kondomu za kike na kiume, upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari, udhibiti wa maambukizi ya virusi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, kutibu magonjwa ya ngono, usalama wa damu waongezwayo wagonjwa hospitalini na upatikanaji wa dawa za kurefusha maisha ya watu waishio na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kutoa huduma zilizo bora kabisa inabidi kuwajengea uwezo watoaji wa huduma za afya kwa kuwapatia mafunzo kwa mfano, pale ambapo huduma mpya imeanzishwa. Mafunzo hayo hutolewa kwa mfumo wa warsha ili kuwapa watumishi wa afya nafasi ya kujifunza kwa vitendo. Uendeshaji wa semina au warsha kwa watumishi wa afya au wadau wengine hutumika kama njia ya kuwajengea uwezo kutekeleza afua husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mchakato mzima wa kupambana na VVU/UKIMWI, walengwa ni Watanzania wote wale wanaoishi na VVU na wale wasio na VVU.

Fedha za kudhibiti UKIMWI zinatekeleza afua za kudhibiti UKIMWI ambazo zinalenga kuwafikia Watanzania wote, wale ambao hawajaathirika pamoja na wale ambao wanaishi na virursi vya UKIMWI. Watanzania wote wale ambao hawajaathirika na virusi vya UKIMWI pamoja na wale ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI. Watanzania wote wanalengwa ili wapate habari kuhusu hatua za kujikinga na UKIMWI, wabadilishe tabia.

Wakati huo huo huduma za matunzo na dawa kwa watu waishio na Virusi vya UKIMWI zinaendelea kupanuliwa na kuimarishwa. Tofauti na dhana iliyojengeka kwamba fedha nyingi zinatumika katika semina na warsha. Ukweli ni kwamba katika Bajeti ya mapambano dhidi ya UKIMWI ni asilimia chini ya 3 ndiyo inatumika katika semina na mafunzo kwa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa lishe kwa watu waishio na Virusi vya UKIMWI, Serikali haina uwezo wa kufanya hivyo. Idadi ya watu waishio na Virusi vya UKIMWI hapa nchini ni zaidi ya milioni 1.4 na gharama za kutoa chakula kwa watu wote hao ni kubwa sana. Hata hivyo, Taasisi ya Chakula na Lishe imeandaa kijitabu cha mwongozo kuhusu vyakula vya asili vinavyofaa katika kuboresha afya ya watu waishio na Virusi vya UKIMWI na wananchi wote kwa ujumla. Elimu kuhusu lishe ni moja ya nguzo muhimu katika tiba ya VVU.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu huu unatumika kwenye Makao Makuu na Halmashauri:-

(a) Je, kwa nini huduma hizi zisipelekwe kwenye Kata ili ziwafikie waathirika wenyewe kwa muda muafaka?

(b) Sasa ni miaka miwili tangu ipitishwe Sheria ya UKIMWI; je, kwa nini mpaka leo kanuni hizi hazijatungwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, mafunzo yanayotolewa, yanatolewa kwa watoa huduma na watoa huduma wako katika ngazi zote mpaka ngazi ya vijijini. Kwa hiyo, si kweli kwamba, hizi huduma haziwafikii kwa sababu wanaotoa huduma wako kule katika vituo vya kutolea huduma kwa wananchi na wananchi wenyewe wako huko.

Swali la pili kuhusu Sheria ya UKIMWI; ni kweli tumeipitisha Sheria na sasa hivi kanuni ziko katika hatua za mwisho, zitakuwa tayari ili ziweze kuanza kutumika.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu, *World Bank* imejitoa kabisa katika kutusaidia kuhusiana na fedha za UKIMWI. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu ametueleza kwamba, Serikali haina uwezo wa kusaidia lishe kwa Waathirika wa UKIMWI; na kwa kuwa UKIMWI bado upo na unaendelea na haujapata dawa na wagonjwa watazidi kuwepo; je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kwamba tunakuwa na fedha zetu za ndani ili kuweza kuwasaidia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nimesema kuwa, Serikali haina uwezo wa kuwapa chakula Waathirika wa UKIMWI. Nilichokisema ni kwamba, Serikali kupitia Taasisi yetu ya Lishe, inatoa elimu kwa wananchi ambao wana Virusi vya UKIMWI ili waweze kutumia chakula cha asili badala ya kuwa na dhana ya kuona kwamba ni lazima watumie labda dawa au nini. Sisi kama Serikali, tumetenga kwenye bajeti yetu fedha za kutoa elimu ili wananchi waweze kutumia chakula bora ambacho kinatokana na mazao ambayo tunayazalisha katika maeneo yetu tunayoishi.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Bunge lako linajitahidi sana kutimiza wajibu wake wa kutunga sheria, lakini imeonekana sheria nyingi ambazo zimetungwa katika Bunge hili kwa kupitishwa kanuni zake, huchukua muda mrefu sana kutungwa hivyo kuwepo na ugumu wa utekelezaji wa sheria hizi. Kuna

tatizo gani katika Serikali la kuchelewa sana kutunga kanuni jambo ambalo linadhoofisha sana utekelezaji wa haki katika nchi?

**SPIKA:** Sina hakika kama ni Wizara ya Afya; pengine Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu atusaidie.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Iwapo Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani anaulizia kanuni ambazo zinahusu Sheria ya Kupambana na UKIMWI au Sheria Iliyoanzisha Kamisheni ya UKIMWI (*TACAIDS*), napenda kukuhakikishia kwamba, kanuni zinaandaliwa, ikiwa ni pamoja na kanuni ya kuwa na Mfuko wa Wadhamini *(Trust Fund)*, kwa kuweka fedha ambazo zitakuwa zinatumika iwapo wafadhili mbalimbali watajitoa katika Mapambano Dhidi ya UKIMWI.

**SPIKA:** Tunaendelea na utaratibu ule ule wa rafiki zetu wa Kambi ya Upinzani.

Na. 24

**Vyuo Kuchelewesha Utoaji wa Vyeti kwa Wahitimu**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwanafunzi anaposoma hutegemea kupata cheti ili kimsaidie kupata ajira au kupandishwa hadhi:-

Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge ni kwa nini baadhi ya vyuo vinachelewa sana kutoa vyeti kwa wahitimu?

**SPIKA:** Ninyi mmependelewa siyo? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya vyuo huchelewa kutoa vyeti kwa wahitimu wao kwa sababu mbalimbali. Moja ya sababu ya ucheleweshwaji wa vyeti hivyo ni kuongeza usalama wa vyeti kwa kuweka alama ambazo si rahisi kuzighushi. Aidha, ili kufikia viwango hivyo vya usalama, baadhi ya Vyuo na Taasisi hizo huchapisha vyeti vyao nje ya nchi.

Hata hivyo, vyuo hutoa *transcript* inayoonesha kiwango cha elimu, shahada iliyopatikana na ubora wake ili kuwasaidia wahitimu wapate kazi kabla vyeti havijatolewa.

Kwa vyuo vinavyochapisha vyeti nje ya nchi, huchukua aghalabu miezi sita kwa wahitimu kupewa vyeti vyao. Vyuo vinavyochapisha hapa nchini hutoa vyeti vya wahitimu wakati wa mahafali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa hapa nchini na hali ya kiusalama kuimarika zaidi, vyuo vingi kwa sasa vina mpango wa kuchapisha vyeti vyao hapa nchini. Kwa kufanya hivyo, wahitimu wataweza kupewa vyeti vyao wakati wa mahafali.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kuwa ni kweli kuna ucheleweshaji wa vyeti hivi vya wahitimu; na kwa kuwa katika maelezo yake amesema hata vile vinavyotengenezwa nje ya nchi vinachukua muda wa miezi sita:-

(a) Je, kwa nini kuna wanafunzi waliomaliza mwaka 2008 Chuo cha CBE mpaka leo hawajapata vyeti vyao? Suala hili nina uhakika nalo kwa sababu nimewauliza wahitimu wenyewe wameniambia mpaka leo hawajapata vyeti.

(b) Je, ni mwezi gani wanafunzi hao watapewa vyeti vyao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, Chuo cha CBE hakiko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kipo chini ya Wizara tofauti.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika jibu letu la msingi tumesema kwamba, zipo sababu mbalimbali ambazo zinafanya mwanafunzi asipewe cheti chake wakati wa kuhitimu mafunzo. Haya ni pamoja na kuongeza alama za usalama, lakini pia kama mwanafunzi ametimiza masharti yote ya kuhitimu katika chuo hicho, kwa mfano, mwanafunzi anaweza asipewe cheti kwa sababu hajakamilisha ada na madai yote ya shule. Sasa kama kuna wanafunzi ambao tangu mwaka 2008 hawajapata vyeti, suala hili tutalifuatilia ili tujue ni nini na kama kuna tatizo tuweze kulitatua mara moja.

**MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge lako Tukufu lilitunga sheria kwamba mwanafunzi yeyote ambaye hajapitia *Law School* hawezi kuajiriwa na kwa kuwa *Law School* imeanza sasa ni *batch* nne wanafunzi waliopitia *Law School* hawajapata vyeti. Watanzania hawa walio wengi wamemaliza Chuo Kikuu kwa gharama kubwa na sasa wako mitaani kwa sababu sheria inawakataza. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa kitu hiki ambacho imetunga sheria na yenyewe inashindwa kuwapa haki

hawa Watanzania ambao kwa fedha za wazazi wao wamejigharimia na hela kidogo ya Serikali lakini wanashindwa kuajiriwa kwa kutokuwa na vyeti?

**SPIKA:** Pengine Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Slaa, kama ifuatavyo:-

*Law School* ni sehemu ya mafunzo ya wanafunzi wote wanaotoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo Kikuu cha Iringa, waliosoma sheria. Wakimaliza kusoma chuoni wanalazimika kuendelea na masomo ya vitendo na haya yanafanyika pale *Law School*. Kwa hiyo, ni sehemu ya mafunzo yao. Ukimaliza Chuo Kikuu hujamaliza mpaka umalize *Law School* ndiyo unakuwa umemaliza kusomea taaluma ya sheria. Sasa tatizo la ajira ni tatizo la watu wengi tu siyo *law* peke yake. Ukifaulu *Law School* unapata cheti, usipofaulu hutapata cheti. Waliofaulu wote wana vyeti; hiyo mimi ninaweza kukuhakikishia

**MBUNGE FULANI:** Naomba ufuatilie hiyo *issue*.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Hapana, nafahamu kwa hakika wote waliofaulu *Law School*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wewe jibu tu usijali bugudha hizi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Kwa hiyo, nataka kusema, kwanza, *Law School* ni lazima na ni muhimu na ukimaliza kama umefaulu utapata cheti chako halafu utakwenda kutafuta ajira.

**SPIKA:** Tunaendelea na utaratibu ule ule wa siku ya Vyama vya Upinzani.

Na. 25

**Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Kila Wilaya Nchini**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Katika kipindi cha Kampeni za Urais, Ubunge na Udiwani, kupitia Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi kuwa Serikali ya Awamu ya Nne itajenga Vyuo vya Ufundi katika kila Wilaya Nchini;-

Je, ni vyuo vingapi vimeshajengwa hadi sasa hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ya Awamu Nne imekaribia kumaliza kipindi chake?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005, ilitoa ahadi ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila

Wilaya na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Shain, alipokuwa katika Kampeni za Urais huko Mkoa wa Manyara alikuwa akiinadi Ilani hiyo ya CCM kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi iliyotolewa, Serikali iliweka kipaumbele kwa Wilaya 28 ambazo hazina aina yoyote ya Chuo cha Ufundi Stadi. Aidha, Serikali ilijenga na kuimarisha Vyuo vya Ufundi Stadi vitano ambavyo ni *Songea VTC, Njiro VTC, Singida VTC, Kigoma VTC* na *Sumbawanga VTC*. Vile vile vyuo vinne vinaendelea kujengwa katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Dar es Salaam na Lindi. Pia ujenzi wa Chuo cha Wilaya ya Makete unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa andiko la mradi kwa ajili ya kutafuta ufadhili wa ujenzi wa Vyuo vingine katika Wilaya ambazo kwa sasa hazina vyuo vya aina hiyo. Katika kipindi hiki ambacho Serikali inakamilisha mpango wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya, mpango wa kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)*, kutoa mafunzo ya Ufundi Stadi unakamilishwa. Lengo ni kuimarisha upatikanaji wa mafunzo ya ufundi stadi kwa wananchi wengi.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005; je, Serikali haioni imepoteza mwelekeo wa kutawala katika nchi hii? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa swali rahisi kabisa hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema, tayari tumeshaanza maandalizi yote ya kujenga hivyo. Kwa hakika, utawala siyo vyuo vya ufundi tu, kwa hiyo, tunaendeleza na tutamaliza kwa sababu Ilani bado inaendelea mwezi haujaisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpango wa Serikali ni mzuri wa kujenga Vyuo vya VETA kila Wilaya iwe na Chuo cha VETA; na kwa kuwa hivi sasa kuna baadhi ya Wilaya kwa mfano Wilaya ya Mpwapwa kuna Chuo cha Maendeleo ya Wananchi; je, Serikali itakuwa tayari kuimarisha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa mfano kile cha Salu ili kiweze kutoa mafunzo kama Vyuo vya VETA? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA KABAKA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, Serikali imeshawasiliana na Wizara husika ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, mipango ni mingi lakini nia ni kuhakikisha kwamba, tunatumia vyuo hivi kama Vyuo vya *VTC* katika kuhakikisha kwamba, wananchi wengi hasa vijana wetu wanapata ufundi stadi katika baadhi ya vyuo hivyo. Kwa hiyo, tutakapokuwa tumekamilisha mipango hiyo, kwa uhakika Chuo cha Mpwapwa kitafikiwa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chama cha Mapinduzi hakikulazimishwa na mtu kuweka ahadi kwenye Ilani ya kujenga Vyuo vya

VETA kila Wilaya; na kwa kuwa mpaka sasa Waziri na kwa maana hiyo Serikali amekiri kwamba wamejenga Vyuo vitano tu kati ya Wilaya zaidi ya 130 zilizoko nchini; na kwa kuwa Waziri anasema kwamba bado maandalizi ya kujenga yanaendelea: Je, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inahitaji miaka mingapi ili kukamilisha maandalizi?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**: Mheshimiwa Spika, katika ujenzi wa Vyuo vya VETA katika Wilaya, tumejiwekea taratibu za kazi hii na katika hatua ya kwanza, Vyuo vitano ambavyo vimetajwa vimekamilika. Wilaya 28 zimetenga maeneo ya ujenzi, michoro yote ya Vyuo hivyo imekamilika na Vyuo thelathini na tano vya *FDCs* vimetayarishwa na kazi inaendelea ya kuvigeuza viwe *VTCs*. Kwa hiyo, Serikali iko kazini na kazi hii inaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Zitto Kabwe kwamba, kwa kuwa CCM itashinda uchaguzi unaokuja, kazi hii itakamilika katika kipindi kijacho cha Bunge hili. *(Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali sasa umekwisha na maswali yote yamejibiwa, kama kawaida kutakuwa na matangazo mafupi. Tunaanza na wageni wetu waliopo Bungeni asubuhi hii, nitaanza na wageni wa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, ambao ni kama ifutavyo: Bibi Khalda Mkulo, Mkewe Waziri, nadhani atakuwa *Speaker's Gallery*. Ahsante sana, tunakushukuru Mama Mkulo kwa kumtunza Mzee, ana kazi ngumu sana kushikilia bajeti katika wakati mgumu kama huu na ujitahidi kuwa karibu nae zaidi ili mambo ya fedha yaendelee kukaa vizuri katika nchi yetu.

Ndugu Jaffer Machano, shemeji yake Waziri, ahsante sana Bwana Jaffer. Ndugu Odilia Martin, shemeji yake na Ndugu Astrida Peter, shemeji yake. Karibuni sana familia ya Mheshimiwa Waziri.

Tunao wageni 54 wa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, ambao wanahudhuria kozi fupi ya uboreshaji mafunzo kwa vitendo katika Vyuo vya Ufundi Stadi Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Manyara, Singida na Dodoma. Wale wenzetu walioko katika Vyuo hivi, wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Kabaka naomba msimame, upande huu na upande ule. Karibuni sana, tunawatakia mema katika kujiendeleza katika mafunzo mzidi kupata mafanikio kwa faida ya nchi yetu. Ahsante sana.

Yupo mgeni wa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe, ambaye ni Ndugu Jenerali Ulimwengu, Mwandishi na mchambuzi nguli wa masula ya siasa, uchumi na jamii; yule pale. Karibu sana Jenerali, kalamu yako ni nzuri, natumaini kwa leo kuangalia mambo yalivyo hapa, makala zitakazofuata basi zitakuwa na uchambuzi ule ule makini tuliouzoea.

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Suzan Lyimo, ambao ni Viongozi wa CHADEMA, Tawi la Chuo Kikuu Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Oraphy Mwinuka.

Naomba wale wa UDOM CHADEMA wasimame; wale pale. Karibuni sana Viongozi wa CHADEMA wa Chuo Kikuu, tunawatakia mema katika masomo, wakati huu msifanye jitihada kujielimisha mambo ya chama haya, zameni katika vitabu, haya ya chama yatakuja baadae. *(Kicheko*)

Tunae mgeni wa Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera, ambaye ni mwanae anayetoka Marekani; sijui anasoma au anafanya kazi Marekani? Ndugu William J. S. Malecela yule pale, karibu sana. Basi ukishachuma huko urudi Mtera na kuwekeza mambo mbalimbali pale.

Ninafurahi kuwajulisha kuwa tunae pia Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais (Tume ya Mipango), Dokta Philip Mpango, akiongoza Ujumbe wa Viongozi Wakuu wa Tume hiyo; dokta ahsante sana. Tunakukaribisha sana Dokta Mpango, kilio cha Waheshimiwa Wabunge wengi imekuwa ni kwamba, tuwe na Tume ya Mipango yenye nguvu, itakayoweza kuainisha jinsi sekta mbalimbali zinavyoweza kuchangia kwa pamoja na kwa mpagilio mzuri na kuleta ufanisi katika uchumi wetu.

Wapo wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Southern Highlands School ya Mufindi; naomba wasimame ni wale pale, karibuni sana. Vijana nadhifu kabisa wa Shule ya Southern Highlands Mufindi, tunawakaribisha sana hapa Dodoma, nadhani mtaendeleza mafanikio ya shule yenu ambayo imeanza kupata umaarufu mkubwa hapa nchini. Hongera kwa walimu na vijana, mfanye kazi kwa bidii, ahsante sana.

Matangazo mengine; kutakuwa na huduma ya clinic ya kutibu vidonda vya tumbo, huduma hiyo inatolewa na Dokta Rahabu Rubago, akifuatana na wasaidizi wake saba. Ninadhani ni vizuri muiulize *Secretariat,* wale wote wanaohisi dalili za vidonda. Waheshimiwa Wabunge kama unahisi una dalili za vidonda na si ajabu kwa wakati kama huu kuwa navyo, basi ni vizuri ili mambo yasiharibike kabisa, maana naambiwa vikizidi hivyo unashindwa hata kusimama. Sasa ni vizuri kumwona Dokta Rahabu Rubago wa *Rahabu Ulcer Clinic Center, Dar es Salaam,* wanatoa huduma zao. Kwa kawaida, huwa tunawapangia ghorofa ya pili, Jengo la Msekwa, lakini sina hakika wako wapi, basi mpate huduma hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Fedha na Uchumi, imeandaa utaratibu wa wataalamu wake wa masuala ya fedha na uchumi, kuwepo katika Ukumbi wa Pius Msekwa mara baada ya maelezo au taarifa na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Hali ya Uchumi wa Nchi yetu.

Kwa hiyo, wataalamu hawa wanaweza kufuatwa pale ili kupata ufafanuzi zaidi wa taarifa itakayosomwa na Mheshimwa Waziri wa Fedha na Uchumi. Hayo ndiyo matangazo ya leo. Sasa namwita Katibu kwa shughuli inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2010 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa ajili ya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Nchi yetu.

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2009 na Mwelekeo katika Muda wa Kati kwa kipindi cha mwaka 2010/11 – 2012/13. Pamoja na Hotuba hii, nawasilisha Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2009; na Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, kwa kutupatia ushauri na maelekezo wakati wa kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2009. Mchango wa Kamati hii siku zote umekuwa na umuhimu wa pekee katika kuboresha Taarifa ya Hali ya Uchumi na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kuwashukuru Naibu Mawaziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee (Mbunge) na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari (Mbunge); Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhani Mussa Khijjah; Naibu Makatibu Wakuu: Ndugu John Michael Haule, Ndugu Laston Thomas Msongole na Dkt. Servacius Beda Likwelile; Makamishna; Wakurugenzi; Viongozi Wakuu wa Asasi zilizo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, ambao wamefanya kazi kwa bidii na kufanikisha kukamilisha Taarifa hii. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru kwa pekee, Profesa Beno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, kwa msaada maalum ambao amekuwa akitupatia. Pia, napenda kuwashukuru Viongozi na Wafanyakazi wenzetu wa Wizara, Mikoa, Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika ya Umma na Taasisi, kwa ushirikiano wao wakati wa kuandaa Taarifa hii. Vile vile, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, kwa kuchapisha Hotuba hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Dkt. Philip Mpango, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Katibu Mtendaji wa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango. Kabla ya kushika wadhifa huu, alikuwa Naibu Katibu Mkuu katika Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, napenda kuwapongeza Makatibu Watendaji Wasaidizi walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa zao katika Tume hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu. Wabunge hao ni Mheshimiwa Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene kutoka Chama cha Mapinduzi (CCM); na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kutoka Chama cha Wananchi

(CUF). Aidha, napenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, kwa kushinda Uchaguzi Mdogo na kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Biharamulo Magharibi kwa tiketi ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na familia ya Mheshimiwa Mbunge mwenzetu aliyefariki katika kipindi hiki, Mheshimiwa Sigfrid Seleman Ng'itu, aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2010, kwa mara ya kwanza kwa Ukanda wa Nchi za Afrika Mashariki na Kati, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 20 wa Uchumi Duniani kuhusu Afrika *(World Economic Forum for Africa - WEFA[1]).* Pamoja na masuala kadhaa yaliyojadiliwa, mada kuu ya mkutano huu ilikuwa ni kutafakari mikakati ya kukuza uchumi kwa Bara la Afrika, kufuatia athari za mtikisiko wa uchumi duniani. Aidha, mkutano ulijadili changamoto zinazolikabili Bara la Afrika na mambo yanayowezesha uchumi kukua, ikiwa ni pamoja na masuala ya kijamii na utawala bora. Watanzania tunatakiwa kufanyia kazi matokeo ya mkutano huo kwa manufaa ya taifa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ilikumbwa na majanga mbalimbali katika mwaka 2009. Katika mwaka huo, kulitokea majanga ya ukame na mafuriko, pamoja na athari za msukosuko wa uchumi duniani, ambayo kwa kiasi kikubwa yaliathiri ukuaji wa uchumi nchini na hivyo kudumaza jitihada za kufikia malengo tuliyojiwekea. Ukame kwenye Mikoa ya Kaskazini lilikuwa ni janga kubwa kwa wafugaji ambapo mifugo yao mingi ilikufa. Aidha, mafuriko yaliyotokea sehemu mbalimbali nchini, zikiwemo Kilosa Mkoani Morogoro, Kongwa, Mpwapwa na Chamwino kwa Mkoa wa Dodoma na maporomoko ya ardhi Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro, yalisababisha watu kufariki, kubomolewa kwa nyumba na miundombinu ya barabara, reli na madaraja. Serikali ilichukua hatua stahili kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa tano tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani. Napenda kueleza baadhi ya mafanikio ya Serikali katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Nne yametokana na kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, MKUKUTA Awamu ya Kwanza, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005. Baadhi ya mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 - 2009, ukuaji wa uchumi umeendelea kuwa imara licha ya athari za msukosuko wa uchumi duniani, kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia na uhaba wa mvua uliotokea katika miaka ya 2005/06 na 2008/09. Katika kipindi hicho, wastani wa ukuaji wa uchumi ulikuwa asilimia 6.9 kwa mwaka, kiwango ambacho bado kilikuwa ndani ya lengo la MKUKUTA la ukuaji wa uchumi wa kati ya asilimi 6 – 8 ifikapo mwaka 2010. Aidha, mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa

na huduma nje yaliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 2,948.3 milioni mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani 4,693.6 milioni mwaka 2009.

Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 2,048.4 milioni mwaka 2005, sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.8 na kufikia Dola za Kimarekani 3,551.3 milioni mwaka 2009, sawa na uwezo wa uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi takribani sita.

Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa matumizi ya kaya (*Household Budget Survey - HBS*[2]) wa mwaka 2007, kiwango cha jumla cha umaskini kimefikia asilimia 33.4 kutoka asilimia 35.7 mwaka 2001.

Vile vile, kwa mujibu wa utafiti wa nguvukazi na ajira *(Intergreted Labour Force Survey - ILFS*[3]*)* wa mwaka 2005/06, watu 760,000 wanaingia katika soko la ajira kila mwaka. Kati ya hao, watu 40,000 wanapata ajira. Lengo ni ukosefu wa ajira ufike asilimia 6.9 mwaka 2010 kutoka asilimia 12.9 ya mwaka 2001, lakini hadi sasa ukosefu wa ajira ni asilimia 11.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa Barabara Kuu na za Mikoa umeongezeka kwa asilimia 19.6 kutoka kilomita 27,603.40 mwaka 2006 hadi kilomita 33,011.98 mwaka 2009. Kati ya hizo, asilimia 52.9 zilikuwa na hali nzuri mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 42.2 mwaka 2006 na zilizokuwa na hali mbaya zilipungua kutoka asilimia 18.5 mwaka 2006 hadi asilimia 13.5 mwaka 2009.

Kuhusu Sekta ya Umeme na Gesi, ilikua kwa wastani wa asilimia 5.7 kati ya mwaka 2006 na 2009 na kuchangia wastani wa asilimia 1.6 katika Pato la Taifa kwa kipindi hicho.

Uzalishaji wa umeme katika Gridi ya Taifa umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka saa za gigawati 1,453.17 mwaka 2006 hadi saa za gigawati 3,290.25 mwaka 2009. Mwaka 2009, wateja wapya 59,547 waliunganishiwa umeme ikilinganishwa na wateja 24,456 mwaka 2007, hivyo kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme kuwa karibu laki moja katika kipindi hicho.

Idadi hii ya wateja waliounganishiwa umeme ni sawa na asilimia 14 ya kaya zote katika maeneo ya mijini ikilinganishwa na asilimia 10 mwaka 2005. Lengo lilikuwa kufikia asilimia 20 mwaka 2010. Kaya zilizounganishiwa umeme vijijini ni asilimia mbili.

Serikali ilianzisha Wakala wa Umeme Vijijini *(Rural Energy Authority)* ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme vijijini.

Pamoja na mafanikio hayo, kumekuwepo na changamoto kadhaa katika sekta hii zikijumuisha kuharibika au kuchakaa kwa miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji; migogoro ya kisheria; uwezo mdogo wa kukidhi mahitaji ya umeme ambayo yanaongezeka kwa wastani wa asilimia 13 – 15 kwa mwaka; na kupungua kwa ujazo wa

maji kwenye mabwawa kulikosababishwa na ukame mwaka 2006 na 2008 ikizingatiwa kuwa karibu asilimia 60 ya umeme unaozalishwa unatokana na maji.

Mheshimiwa Spika, vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka watoto 112 kati ya 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2004/05 hadi kufikia watoto 91 kati ya 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2008/2009.

Aidha, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 68 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2004/2005 na kufikia 58 kati ya watoto 1,000 mwaka 2008/2009. Kiwango halisi cha uandikishaji wa wanafunzi katika shule za msingi kimeongezeka kutoka asilimia 96.1 mwaka 2006 hadi asilimia 97.2 mwaka 2008.

Aidha, kiwango halisi cha uandikishaji kidato cha kwanza hadi cha nne pia kilipanda kutoka asilimia 13.4 mwaka 2006 hadi asilimia 29.1 mwaka 2009. Kadhalika, kiwango cha ukatishaji masomo kilishuka kutoka asilimia 3.4 mwaka 2006 hadi asilimia 3.1 mwaka 2008.

Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 - 24 yamepungua kutoka asilimia 7.4 mwaka 2005 hadi asilimia 5.7 mwaka 2008 na lengo lilikuwa kufikia asilimia 5.0 mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, idadi ya wanawake katika ngazi za maamuzi imeongezeka kutoka 149 mwaka 2007/08 hadi kufikia 218 mwaka 2008/09 ikiwa ni pamoja na uteuzi wa Majaji wanawake, Mawaziri na Wakurugenzi wa Wizara. Demokrasia imeimarika kwa kuendesha chaguzi mbalimbali zikiwemo za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa amani na utulivu na uhuru wa wananchi kutoa maoni umeimarika kwa kuzingatia utawala wa sheria na kutoingilia uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu athari za msukosuko wa uchumi wa Tanzania. Mwaka 2008/09, dunia ilikumbwa na msukosuko wa kiuchumi kufuatia kuanguka kwa masoko ya fedha na mitaji. Madhara ya mtikisiko wa uchumi duniani kwa upande wa Tanzania, yalijitokeza kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2009, ambapo bei za mazao ya biashara (kama vile pamba, korosho, katani, kahawa na maua) katika soko la dunia ziliporomoka na kusababisha makampuni ya ununuzi wa mazao hayo kushindwa kuuza au kuuza kwa hasara.

Hali hii ilipelekea makampuni hayo kukosa uwezo wa kulipa madeni yao kwa wakati uliotakiwa, hivyo kuashiria kuwepo kwa mikopo chechefu (*non-performing loans*) katika sekta ya fedha kutokana na msukosuko huo. Kwa upande wa madini, ni dhahabu pekee ndiyo ilikuwa na soko la uhakika, ambapo bei yake ilipanda kwa asilimia 4.8 na mapato yatokanayo na mauzo yake nje kuongezeka kwa asilimia 18.7 katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, athari nyingine zilizojitokeza kutokana na msukosuko katika uchumi ni kupungua kwa uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja (FDI)1; kupunguzwa

kazi kwa wafanyakazi, hususan kwenye sekta ya utalii; kupungua kwa idadi ya watalii na mapato yatokanayo na utalii; kuongezeka kwa riba za mikopo kutoka nje hivyo kupunguza upatikanaji wake na kupungua kwa mapato ya kodi kutokana na kushuka kwa shughuli za uchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ilifanya jitihada za dhati za kunusuru uchumi kwa kupunguza makali ya madhara yatokanayo na msukosuko huo. Serikali iliandaa Mkakati wa kunusuru uchumi uliokadiriwa kugharimu shilingi trilioni 1.7. Hadi Machi 2010, kiasi cha shilingi bilioni 1,207.5, sawa na asilimia 71.3 ya fedha zilizokadiriwa zilikuwa zimeshatolewa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mkakati huu unagharamia pamoja na mambo mengine, fidia za hasara zilizotokana na msukosuko wa uchumi duniani, uimarishaji mifuko ya dhamana kwa wajasiriamali wadogo na wa kati na utoaji ruzuku kwenye mpango wa ugawaji wa mbolea kwa wakulima. Hata hivyo, tumejifunza mambo mengi, kama vile kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mkakati wa kunusuru uchumi kutokutosha kutokana na mapato ya Serikali kuwa kidogo na hivyo kusababisha idadi ndogo tu ya waathirika kufidiwa. Vile vile kumekuwepo ufahamu na mawasiliano duni kati ya waathirika na benki zao katika kufuata taratibu za kuwasilisha maombi yao Benki Kuu ambayo ilikuwa na wajibu wa kuhakiki maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatathmini mpango mzima wa kunusuru uchumi ili kubaini mafanikio na changamoto katika kutekeleza mpango huo. Hata hivyo, dalili za awali zinaonesha kuwa utekelezaji wa Mpango huu ulileta matunda mazuri kama vile ukuaji wa Pato la Taifa, kushuka kwa mfumuko wa bei na ongezeko la mauzo nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malengo ya mwaka 2009/2010. Mwaka jana wakati nawasilisha hotuba ya Hali ya Uchumi nilibainisha malengo tuliyokusudia kuyafikia katika kipindi cha muda wa kati. Malengo hayo yalizingatia athari za kuyumba kwa uchumi wa dunia. Baadhi ya malengo hayo ni kama haya yafuatayo:-

(i) Pato la Taifa lilitarajiwa kukua kwa asilimia 5.0 mwaka 2009, asilimia 5.7 mwaka 2010 na kuongezeka hadi kufikia asilimia 7.2 mwaka 2011 na 7.5 mwaka 2012;

(ii) Kasi ya upandaji bei ingepungua na kufikia chini ya asilimia 10, mwishoni mwa Juni 2010;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani ambayo yangefikia Pato la Taifa kwa bei ya mwaka husika kwa asilimia 15.9 mwaka 2008/09; asilimia 16.4 mwaka 2009/10; asilimia 17.2 mwaka 2010/11 na asilimia 18.3 mwaka 2011/12;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) katika wigo utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi na kasi ya upandaji bei na kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayowezesha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(v) Kuwa na kiwango cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha; na

(vi) Kuondoa vikwazo vya kimfumo na kimuundo katika sekta ya fedha, ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya mwenendo wa uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2009. Baada ya kusema hayo, sasa naomba nianze kutoa muhtasari wa mapitio ya hali ya uchumi na maendeleo kwa mwaka 2009, ikiwa ni mapitio ya mwaka wa tano na wa mwisho wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA I). Aidha, ikumbukwe kwamba taarifa hii ni ya kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2009 na sehemu chache zimegusa robo ya kwanza ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuaji wa pato la Taifa. Mwaka 2009 uchumi wetu uliendelea kukabiliwa na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani, ingawa dalili za uchumi kuanza kuimarika kutoka katika matatizo hayo zimeanza kuonekana. Pato Halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 6.0 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 7.4 mwaka 2008. Ukuaji huu ni zaidi ya lengo lililorekebishwa la asilimia 5.5. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa viwango vya ukuaji katika shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa umeme na gesi, elimu na utoaji wa huduma za mawasiliano ikijumuisha matumizi ya simu za mkononi. Aidha, mchango wa shughuli za kiuchumi za huduma umeendelea kuongoza katika mwaka 2009, ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukua kwa Pato la Taifa hadi shilingi bilioni 28,212.6 kwa bei za mwaka husika na idadi ya watu Tanzania Bara kukadiriwa kuwa watu milioni 40.7, Pato la Wastani la kila Mtanzania liliongezeka hadi shilingi 693,185 mwaka 2009, ikilinganishwa na shilingi 628,259 mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 10.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, napenda nielezee kwa kifupi ukuaji wa uchumi katika sekta mbalimbali ingawa Mawaziri wa maeneo husika wataeleza kwa kina maendeleo katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za kilimo, mifugo, misitu na uwindaji kilikuwa asilimia 3.2 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 4.6 mwaka 2008. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji katika shughuli hizi kulitokana na uhaba wa mvua na ukame katika baadhi ya maeneo hasa kaskazini mwa nchi. Hali hii ilisababisha uzalishaji wa mazao kupungua na mifugo kukosa malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hayo, kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za uzalishaji mazao kilishuka kutoka asilimia 5.1 mwaka 2008, hadi asilimia 3.4 mwaka 2009. Mazao ambayo uzalishaji wake ulipungua yanajumuisha chai, tumbaku, mahindi, mtama/ulezi na mihogo. Kiwango cha ukuaji katika shughuli ndogo za mifugo

kilipungua kutoka asilimia 2.6 mwaka 2008, hadi asilimia 2.3 mwaka 2009. Kwa upande wa shughuli ndogo za kiuchumi katika misitu na uwindaji, kiwango cha ukuaji kiliongezeka hadi asilimia 3.5 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 3.4 mwaka 2008. Hii ilitokana na kuimarika kwa doria kwenye maeneo ya uvunaji, usafirishaji na masoko ya mazao ya misitu na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya misitu katika soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi za uvuvi kilikuwa asilimia 2.7 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 5.0 mwaka 2008. Kupungua kwa kiwango hiki kulitokana na kuendelea kutumia zana duni za uvuvi, uharibifu wa mazalia ya samaki na kuongezeka kwa ushindani katika soko la Ulaya hasa kutoka katika nchi za China na Vietnam wanaotumia utaalam wa kisasa katika kufuga na kuzalisha samaki. Hata hivyo, mchango wa shughuli za uvuvi katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 1.2 mwaka 2008 na kufikia asilimia 1.4 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda na ujenzi. Kiwango cha ukuaji wa uzalishaji bidhaa viwandani kilikuwa asilimia 8.0 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 9.9 mwaka 2008. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa kama vile konyagi, mabati, chibuku na unga wa ngano. Mchango wa shughuli za uzalishaji bidhaa viwandani katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.6 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 7.6 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za ujenzi zilikua kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na asilimia 10.5 mwaka 2008. Ukuaji huo ulichangiwa hasa na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi wa barabara na madaraja, majengo ya kuishi na yasiyo ya kuishi na uendelezaji wa ardhi. Mchango wa shughuli za ujenzi katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.9 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 7.7 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi kiliongezeka hadi kufikia asilimia 8.4 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 5.4 mwaka 2008. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme wa gesi na makaa ya mawe. Katika mwaka 2009 shughuli za kiuchumi katika umeme na gesi zilichangia asilimia 1.7 katika Pato la Taifa kama ilivyokuwa mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji katika shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe kilikuwa asilimia 2.5 mwaka 2008, ikilinganishwa na asilimia 1.2 mwaka 2009. Kushuka kwa kiwango cha ukuaji kulitokana na kushuka kwa bei za *Tanzanite* na almasi katika soko la dunia na kupungua kwa uzalishaji wa dhahabu katika migodi ya Tulawaka na *Resolute* kufuatia kushuka kwa daraja la mashapo (*ore grade*) ya dhahabu. Mchango wa shughuli za kiuchumi za madini na uchimbaji mawe katika Pato la Taifa ulipungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2008, hadi asilimia 3.3 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utoaji huduma zinajumuisha biashara na matengenezo, uchukuzi, mawasiliano; hoteli na migahawa; utawala; elimu; afya; huduma za fedha na bima na upangishaji wa majengo. Kiwango cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika utoaji huduma kilikua kwa asilimia 7.2 mwaka 2009 ikilinganishwa na

asilimia 8.5 mwaka 2008. Mchango wa shughuli za utoaji huduma katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 43.6 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 43.8 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi za mawasiliano katika mwaka 2009 zilikua kwa kiwango cha juu zaidi, ikilinganishwa na shughuli nyingine za kiuchumi. Kiwango cha ukuaji cha shughuli hizi kilikuwa asilimia 21.9 mwaka 2009 ikilinganishwa na asilimia 20.5 mwaka 2008. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya mawasiliano, kuongezeka kwa wateja wa simu za mkononi na mauzo ya vocha za simu. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.1 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 2.5 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kiuchumi katika huduma za uchukuzi zilikua kwa kiwango cha asilimia 6.0 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2008. Hii ilitokana na kushuka kwa ufanisi kufuatia uchakavu na ukosefu wa vitendea kazi (ikiwemo mabehewa na ndege) vya usafirishaji wa mizigo na abiria kwa njia ya anga na reli hususan kwa makampuni ya Reli na Shirika la Ndege la Tanzania. Hata hivyo, mchango wa huduma za uchukuzi katika Pato la Taifa umeongezeka na kuwa asilimia 5.2 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, shughuli ndogo za mahoteli na migahawa (ikijumuisha utalii) zilikua kwa asilimia 4.4 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2008. Ukuaji huo ulitokana na kupungua kwa idadi na kiwango cha matumizi ya watalii, kufuatia hali ya kuyumba kwa uchumi wa dunia na msukosuko wa soko la fedha na mitaji. Mchango wa shughuli ndogo za huduma za mahoteli na migahawa katika Pato la Taifa ulishuka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2008 hadi asilimia 2.3 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009, kasi ya upandaji bei za bidhaa na huduma iliendelea kuwa tarakimu mbili, ambapo wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 12.1, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 10.3 mwaka 2008. Hii ilitokana na uhaba wa chakula uliotokea nchini na katika nchi za jirani uliosababisha kupanda kwa bei za mazao ya chakula. Aidha, bei ya bidhaa za mafuta katika soko la ndani ilipanda na hivyo kuongeza gharama za usafirishaji.

Hata hivyo, kuanzia Oktoba mwaka 2009, mwelekeo wa mfumuko wa bei ya chakula ambao ndio huchangia kwa kiasi kikubwa wastani wa jumla wa kasi ya upandaji bei ulianza kushuka kutoka asilimia 18.1, hadi asilimia 9.8 Aprili mwaka huu, sawa na kushuka kwa karibu nusu, kutokana na kuwepo kwa mvua katika maeneo mengi ya Ukanda wa Afrika Mashariki na hivyo kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula. Hali hii pia iliwezesha kushuka kwa wastani wa jumla wa kasi ya upandaji bei, kutoka tarakimu mbili za asilimia 12.7 mwezi Oktoba mwaka 2009, hadi asilimia 9.4 mwezi Aprili mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kukujulisha kwamba leo Wataalam wangu wamenijulisha kwamba mwezi wa tano mfumuko wa bei ulishuka na kufikia asilimia 7.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 10.7 hadi shilingi bilioni 8,173.2 mwaka 2009. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulikuwa asilimia 29.0, ikilinganishwa na asilimia 29.7 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, ukuzaji rasilimali katika sekta ya umma (ikijumuisha Serikali kuu, taasisi na mashirika) uliongezeka kutoka shilingi bilioni 1,929.4 mwaka 2008 hadi shilingi bilioni 2,241.5 mwaka 2009 kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 16.2. Mchango wa sekta ya umma katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 27.4 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 26.1 mwaka 2008. Ukuzaji rasilimali katika sekta binafsi uliongezeka kutoka shilingi bilioni 5,344.9 mwaka 2008, hadi shilingi bilioni 5,779.5 mwaka 2009, kwa bei za miaka husika, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Mchango wa sekta binafsi katika ukuzaji rasilimali ulikuwa asilimia 70.7 mwaka 2009, ikilinganishwa na asilimia 72.4 mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujazi wa fedha na karadha. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2)2 ulikua kwa asilimia 23.4 katika mwaka ulioishia Januari 2010, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 22.0 Januari 2009. Vile vile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 20.8 ikilinganishwa na asilimia 17.7 katika kipindi kama hicho. Kwa upande wa thamani ya shilingi ya Tanzania kwa Dola ya Kimarekani iliendelea kushuka kutoka sh 1,196.3 kwa Dola mwaka 2008, hadi shilingi 1,320.3 mwaka 2009. Hii ni sawa na kupungua kwa thamani kwa asilimia 10.3. Kushuka kwa thamani ya shilingi ya Tanzania kumetokana na watu kuhodhi fedha zao kutokana na kujilinda na msukosuko wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha ukuaji wa mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi kiliendelea kushuka na kufikia asilimia 9.7 Januari 2010, kutoka asilimia 41.0 Januari 2009. Hii ilisababishwa na mabenki kuchukua tahadhari katika utoaji wa mikopo, kwa kuhofia athari za msukosuko wa masoko ya fedha na mitaji duniani.

Mheshimiwa Spika, wastani wa viwango vya riba za mikopo ulipungua hadi asilimia 14.38 Desemba 2009, kutoka asilimia 16.05 Desemba 2008. Wastani wa riba za amana za akiba uliongezeka kutoka asilimia 2.74 Desemba 2008, hadi asilimia 2.83 Desemba 2009. Aidha, riba za amana za muda maalum (mwaka mmoja) ziliongezeka kutoka asilimia 8.48 Desemba 2008 hadi asilimia 8.99 Desemba 2009 na riba za kukopa za vipindi maalum yaani (mwaka mmoja) ziliongezeka kutoka asilimia 13.56 Desemba 2008, hadi asilimia 13.96 Desemba 2009.

Mheshimiwa Spika, kufuatia utekelezaji madhubuti wa awamu ya pili ya program ya maboresho ya sekta ya fedha na azma ya Serikali kuhakikisha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, viwango vya riba za mikopo ya muda mrefu (zaidi ya miaka mitano) vimeendelea kushuka kufikia wastani wa asilimia 13.67 mwezi Desemba 2009, kutoka wastani wa asilimia 16.43 mwezi Desemba 2008.

Vile vile, viwango vya riba za mikopo ya muda wa kati (hadi miezi 24) vilishuka kufikia wastani wa asilimia 15.01 mwezi Desemba 2009, kutoka wastani wa asilimia

16.57 mwezi Desemba 2008 na kwa upande wa riba za amana za muda wa kati yaani (miezi 24) ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 7.56, kutoka wastani wa asilimia 5.75, katika kipindi hicho hicho na hivyo kuendelea kuhamasisha wananchi kuweka fedha zao benki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Nje. Katika mwaka 2009, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 4,687.7 mwaka 2008, hadi Dola za Kimarekani milioni 4,693.6. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa asilia, hususan, korosho, kahawa, tumbaku na karafuu. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa toka nje zilipungua kwa asilimia 7.1 kutoka Dola milioni 8,089.2 mwaka 2008, hadi Dola milioni 7,513.9 mwaka 2009. Hii ilisababishwa na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa za kati, hususan mbolea na mafuta na kusababisha kupungua kwa nakisi ya urari wa bidhaa, huduma na uhamisho mali kutoka Dola milioni 2,883.6 mwaka 2008, hadi Dola milioni 2,208.1 mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 3,551.3 Desemba 2009, kutoka Dola milioni 2,872.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2008, sawa na ongezeko la asilimia 23.6. Kiasi hiki cha akiba ya fedha za kigeni kinatosha kuagiza bidhaa na huduma nje kwa muda wa miezi 5.7.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bajeti ya Serikali. Mapato ya ndani yaliongezeka kwa asilimia 18.1 kufikia shilingi bilioni 4,293.1 mwaka 2008/09, kutoka shilingi bilioni 3,634.6 mwaka 2007/08. Hata hivyo, kiasi hicho kilichokusanywa ni pungufu ya makadirio kwa asilimia 10 kwa mwaka 2008/09. Katika kipindi cha Julai 2009-Machi 2010, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 3,490.3, ikiwa ni asilimia 8.7 chini ya makisio ya shilingi bilioni 3,924.9 kwa kipindi hicho. Upungufu huu ulitokana hasa na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, Misaada na Mikopo ya Nje. Mwaka 2009/10, Serikali ilikadiria kupata shilingi bilioni 1,193.9 kutokana na misaada na mikopo ya kibajeti. Katika kipindi cha Julai 2009 hadi Machi 2010, misaada na mikopo ilifikia shilingi bilioni 989.5, sawa na asilimia 98 ya makadirio. Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo ilifikia shilingi bilioni 1,328.8 Machi 2010, sawa na asilimia 93 ya makadirio katika kipindi hicho. Kati ya hizo, misaada ni shilingi bilioni 678.3 na mikopo shilingi bilioni 650.5.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 6,811.8 mwaka 2008/9, sawa na asilimia 95.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 7,192.1. Matumizi ya maendeleo yalikuwa asilimia 14 chini ya lengo. Katika kipindi cha Julai 2009 – Machi, 2010, matumizi ya Serikali yalifikia shilingi bilioni 6,143.9, ikiwa ni asilimia 91 ya makisio ya matumizi ya shilingi bilioni 6,718.7. Kupungua kwa matumizi hayo kulitokana na upungufu wa mapato katika kipindi hicho. Hotuba yangu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2010/11 nitakayowasilisha baadaye leo, inabainisha kwa kina mwenendo wa mapato na matumizi ya Serikali mwaka 2009/10 pamoja na makadirio kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2009, Deni la Taifa lilifikia Dola za Kimarekani milioni 10,690.3. Kati ya deni hilo, Dola milioni 7,768.1, sawa na asilimia 72.7 ya deni lote ilikuwa deni la nje. Kati ya deni lote la nje, Dola milioni 1,514.6 lilikuwa ni la sekta binafsi, sawa na asilimia 19.5 ya deni lote la nje na Dola million 6,253.5 ilikuwa ni deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho cha deni la nje la Serikali, Dola milioni 5,155.8 (asilimia 82.4) zilikuwa ni bakaa ya deni na kiasi kilichobaki ni malimbikizo ya riba.

Mheshimiwa Spika, hadi Desemba 2009, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 3,837.7. Malipo ya deni la ndani kwa mwaka 2009, yalikuwa shilingi bilioni 773.3.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maboresho ya Sekta ya Fedha. Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya awamu ya pili ya mageuzi ya sekta ya fedha, utekelezaji ambao ulianza rasmi mwaka 2006/07. Utafiti uliofanywa hivi karibuni unaonesha kuwa kuna maendeleo na uhimilivu katika sekta ya fedha. Matokeo ya awali ya utafiti huo pia yanaonesha kuwa mitaji ya benki haijaathirika japo kulikuwepo na ongezeko dogo la mikopo chechefu iliyotokana na athari za kuyumba kwa uchumi wa dunia. Benki za nje zenye matawi hapa nchini zinafuata sheria na taratibu za hapa nchini ndio maana katika awamu ya kwanza hazikuathirika kutokana na kuyumba kwa masoko ya fedha na mitaji duniani.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya kazi zilizofanyika mwaka 2009 kupitia mradi wa maboresho ya sekta ya fedha ni pamoja na Serikali kuibadili Benki ya Rasilimali Tanzania kuwa Benki mahsusi kwa ajili ya kutoa mikopo ya muda mrefu. Katika mwaka 2008/09, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi 27 bilioni kwa ajili ya kuongeza mtaji wa Benki. Vile vile, Serikali iliendelea kuandaa usimamizi na namna bora ya kugeuza mifuko ya dhamana ili iwe inajitegemea na kuwa endelevu. Serikali inaendelea na majadiliano kuangalia namna ya kuboresha mifuko ya dhamana.

Serikali pia inaendelea na mchakato wa kuanzisha *Credit Reference Data Bank* na kuanzisha ofisi itakayoshughulika na masuala ya taarifa za mikopo (*Credit Reference Bureau*) kwa lengo la kuwatambua wakopaji wenye sifa stahili na wanaokopesheka na mienendo yao katika kukopa na kurejesha.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha upatikanaji wa fedha za kujenga makazi au kununua nyumba bora na za bei nafuu na kwa kuzingatia umuhimu wa makazi bora, Serikali ilizindua mradi wa mikopo ya nyumba mwaka 2009 ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia kwa mkopo wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 40. Lengo la Mradi huu ni kupanua wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya kununua, kujenga au kukarabati nyumba. Kampuni mahususi kwa ajili ya kutafuta fedha na kutoa mikopo ya muda mrefu ya nyumba (*Tanzania Mortgage Refinance Company – TMRC*) imeshaanzishwa. Mchakato wa kuandaa taratibu za uongozi, usimamizi na mpango kazi wa kampuni hiyo zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ya mwaka 2008 iliyounda Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (*Social Security Regulatory Authority Act*

2008) inaipa Benki Kuu ya Tanzania mamlaka ya kusimamia masuala yote ya fedha yanayohusu Mifuko ya Pensheni. Utekelezaji wa zoezi hili unategemea uanzishwaji wa mamlaka itakayosimamia Mifuko ya Pensheni pamoja na mwongozo wa uwekezaji, ambayo mchakato wake unaendelea chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Serikali pia inajiandaa kutumia mfumo wa malipo wa *TISS* (*Tanzania Inter-bank Settlement System*) unaolenga kuboresha na kuongeza ufanisi katika ulipaji malipo ili kupunguza malimbikizo ya malipo (*expenditure float*).

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuaji wa uchumi duniani. Mwaka 2009, Pato la Dunia lilikua kwa asilimia hasi 0.6, ikilinganishwa na asilimia chanya 3.0 mwaka 2008. Kushuka kwa ukuaji kulitokana na kupungua kwa biashara na uzalishaji duniani, ikiwa ni matokeo ya athari za msukosuko wa kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, Pato la Nchi Zilizoendelea lilikua kwa asilimia hasi 3.2 mwaka 2009, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 0.5 mwaka 2008. Ukuaji wa Pato la Nchi Zinazoinukia Kiuchumi na Zinazoendelea ulishuka hadi asilimia 2.4 mwaka 2009, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.1 mwaka 2008. Kushuka kwa kiwango hiki kulisababishwa hasa na kupungua kwa uwekezaji na uuzaji bidhaa nje, kushuka kwa bei za bidhaa na kupungua kwa mitaji ya moja kwa moja kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika. Mwaka 2009, kiwango cha ukuaji wa Pato la Bara la Afrika kilishuka hadi asilimia 1.9, kutoka asilimia 5.2 mwaka 2008. Pato la Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara lilishuka kutoka asilimia 5.5 mwaka 2008, hadi asilimia 2.1 mwaka 2009. Kushuka huku kulitokana na kupungua kwa uuzaji wa bidhaa nje na uwekezaji wa moja kwa moja. Aidha, msukosuko wa uchumi duniani ni moja ya sababu zilizochangia kushuka kwa viwango vya ukuaji wa uchumi katika nchi nyingi za Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*). Mwaka 2009, Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea na utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Nchi yetu iliridhia kuanzishwa kwa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itifaki hii inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwezi Julai 2010, ikiwa ni hatua ya Pili ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Changamoto iliyopo ni uelewa mdogo wa wananchi juu ya mtangamano wa *EAC* ambao utawafanya kushindwa kutumia vizuri fursa zinazotokana na mchakato wa mtangamano wa *EAC*. Hatua itabidi zichukuliwe haraka kuondoa dosari hii ili wananchi wa Tanzania waweze kushiriki kikamilifu na kufaidika katika soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*). hadi mwishoni mwa 2009, asilimia 85 ya biashara ya bidhaa baina ya nchi za *SADC* imekuwa ikifanyika bila kutozwa ushuru. Aidha, nchi wanachama zinaendelea na mchakato wa kuondoa ushuru wa asilimia 15 katika bidhaa zilizobaki, ili ifikapo mwaka 2012, biashara zote za bidhaa zifanyike bila kutozwa ushuru. Nchi wanachama ambazo hazijajiunga na Soko Huru la *SADC* ni Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Angola, Malawi na Seychelles. Katika eneo hili pia, wananchi inabidi waelimishwe ili kuongeza uelewa wao na kuweza kushiriki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Idadi ya Watu. Mwaka 2009, idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa milioni 41.9, kulingana na kiwango cha ukuaji wa idadi ya watu cha asilimia 2.9 cha Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002. Kati ya hao, wanawake walikuwa milioni 21.3, sawa na asilimia 50.8 na wanaume milioni 20.6, sawa na asilimia 49.2. Idadi ya watu Tanzania Bara ilikuwa milioni 40.7 ambapo Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu milioni 1.2. Mgawanyo wa watu unaonesha kuwa watu milioni 31.1, sawa na asilimia 74.3 ya watu wote wanaishi vijijini wakati watu milioni 10.8 wanaishi mijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na nguvukazi na ajira, mwaka 2009, nguvukazi nchini ilikadiriwa kuwa watu milioni 21.9, sawa na asilimia 52.2 ya watu wote. Msukosuko wa Uchumi wa Dunia umeathiri nyanja nyingi za kiuchumi ikiwa ni pamoja na shughuli za utalii, kilimo na soko la ajira, na hivyo kuongeza upungufu wa ajira hapa nchini. Inakadiriwa kuwa asilimia 30 ya watembeza watalii (*tour guides*) wamepoteza ajira zao hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2009. Aidha, ajira katika sekta ya kilimo hususan kilimo cha maua kilishuka kwa asilimia 15 katika mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Utawala Bora. Mwaka 2009, katika kutekeleza mpango wa kutenganisha shughuli za polisi za upelelezi na kuendesha mashtaka, Serikali iliongeza ofisi tatu za kanda katika mikoa ya Shinyanga, Lindi na Mara. Aidha, Mawakili wa Serikali 250 waliajiriwa ili kuongeza ufanisi katika kuendesha mashtaka katika ngazi za Wilaya. Vile vile, katika kufanikisha azma ya Serikali ya kuongeza mapambano dhidi ya rushwa, kesi kubwa 15 za rushwa zilifunguliwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika harakati za kupambana na uharibifu wa mazingira, Serikali iliendelea kutekeleza sera, mikakati, sheria na kanuni za usimamizi wa mazingira, ili kunusuru uchumi na maendeleo endelevu ya nchi kwa ujumla. Mwaka 2009, kanuni tatu za mazingira ambazo ni Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa, Usimamizi wa Taka Ngumu na ile ya Usimamizi wa Taka Sumu ziliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vita dhidi ya UKIMWI. Janga la UKIMWI limeendelea kuwa na athari katika jamii. Katika mwaka 2009, Serikali iliendelea kuboresha huduma za tiba kwa wanaoishi na Virusi Vya UKIMWI (VVU) kwa kuhakikisha kuwa dawa za kupunguza makali ya VVU zinapatikana katika vituo vya kutoa huduma. Idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na ambao wanapata dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, iliongezeka hadi watu 284,227 mwaka 2009, kutoka 208,579 mwaka 2008. Kati yao, watoto walio na umri chini ya miaka 15 walikuwa 20,959.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jinsia. Mwaka 2009, Serikali imeendeleza jitihada za makusudi katika kuhakikisha uwakilishi zaidi wa wanawake katika ngazi za kufanya maamuzi, yaani uongozi. Ili kufanikisha azma hii, Serikali ilidhamini maafisa wanawake 221 kusoma shahada za uzamili katika vyuo vya ndani na nje ya nchi. Aidha, hatua kubwa imefikiwa katika uwakilishi wa wanawake katika ngazi za wizara na idara

mbalimbali; idadi hii iliongezeka kutoka wanawake 149 mwaka 2007/08 na kufikia jumla ya wanawake 218 katika mwaka wa 2008/09.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ina malengo ya kuwaletea wananchi maisha bora na mazuri, kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria na kujenga uchumi imara wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani. Tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 iliyofanyika mwaka 2009, ilibainisha upungufu uliojitokeza katika utekelezaji na kutoa mapendekezo ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kufikia malengo ya Dira. Tathmini hiyo ya mshauri elekezi ilibainisha kwamba dhana ya Dira bado ni sahihi na inatekelezeka kama kutaongezwa msukumo katika utekelezaji.

Tathmini hiyo pia ilitoa changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na haja ya kuainisha hatua ya utekelezaji kisekta iliyofikiwa hadi sasa ikilinganishwa na malengo ya awali ya Dira na kuitangaza ili ieleweke kwa wadau. Aidha, tathmini ilibainisha haja ya kuwa na mfumo linganishi wa utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya muda wa kati na mrefu. Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango inazifanyia kazi changamoto hizo, kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) ulianza mwaka 2005/06 na utakamilika ifikapo mwisho wa Juni 2010. Tathmini ya utekelezaji wa MKUKUTA imeainisha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya MKUKUTA kwa kuchambua mafanikio na changamoto. Taarifa ya utekelezaji wa MKUKUTA imeelezwa kwa undani katika taarifa ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya mwaka 2009 (*PHDR* 2009), Taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa MKUKUTA ya mwaka 2009 na tarifa za tafiti za kisekta.

Mheshimiwa Spika, takwimu za utafiti wa matumizi ya kaya wa mwaka 2007 zinaonesha kuwa mafanikio yaliyopatikana katika ukuaji uchumi tangu mwaka 2001 hayajajibainisha vya kutosha katika kupunguza umaskini wa kipato. Hali hii inatokana kwa kiasi kikubwa na ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo yenye kuajiri watu wengi zaidi hasa maskini. Hivyo, changamoto ni kuboresha uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo na kuwawezesha wananchi ili kuongeza kipato chao na kujiletea maendeleo yao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa maandalizi ya MKUKUTA Awamu ya Pili yaliyoanza Mwezi Januari Mwaka 2009, umekamilika. Mchakato huu umehusisha wadau mbalimbali ikiwemo Serikali, Waheshimiwa Wabunge, mashirika yasiyo ya kiserikali, wanataaluma, watafiti, mashirika ya dini, wahisani, vyama vya wafanyakazi na sekta binafsi. Mara baada ya kupitishwa na Serikali, MKUKUTA II utaanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2010/11.

Mheshimiwa Spika, MKUKUTA II unalenga katika misingi mikuu minne, ambayo ni:

(i) Kuendeleza na kuhakikisha matumizi bora ya njia kuu za uzalishaji ikiwemo raslimali watu, ardhi, na mtaji;

(ii) Kujenga na kuimarisha mifumo ya kiuchumi, hii ikiwa inalenga katika kujenga taasisi muhimu za kujenga na kusimamia uchumi na ustawi wa jamii;

(iii) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya uchumi ikijumuisha nishati hasa umeme, maji, barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege; na

(iv) Kuimarisha usimamizi wa uchumi, hasa katika kujenga uwezo wa Serikali katika kuwezesha sekta binafsi na sekta nyingine ili zishiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, tofauti na ilivyokuwa katika MKUKUTA I, MKUKUTA II utazingatia masuala ya msingi katika uratibu ulioboreka kuharakisha kufikia matokeo; kubuni mikakati ya muda mrefu; kuweka vipaumbele vichache vitakavyotekelezeka, kunufaisha wengi na kutuwezesha kufikia matokeo tarajiwa na kuimarisha mikakati ya utekelezaji wa programu za maboresho na programu au miradi mbalimbali ya kisekta na za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009, Serikali iliendelea kuchukua hatua za makusudi katika kuimarisha na kuendeleza sekta binafsi, ikiwa ni pamoja na kuandaa Sera na kukamilisha maandalizi ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPP)*. Kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara kupitia programu mbalimbali kama vile MKUMBITA na Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi *(PSDS)*. Hata hivyo, Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2009, inaonesha kuwa gharama za ufanyaji biashara nchini bado ni kubwa, kwani nafasi ya Tanzania katika vigezo vya kupima urahisi wa kufanya biashara imeshuka kutoka nafasi ya 126 kati ya nchi 183 mwaka 2008 na kuwa ya 131 mwaka 2009. Hivyo, hatua zaidi zinachukuliwa kupunguza vikwazo vya kufanya biashara nchini na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009, Awamu ya Pili ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, ilitoa mikopo yenye thamani ya Tshs. bilioni 2.3. Fedha hizo zilitolewa katika Wilaya 21 ambazo hazikupata katika awamu ya kwanza na Wilaya 46 zilizopata chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009, Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.428 kwa *SACCOS* kupitia Benki ya *CRDB* katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, Singida na Rukwa. Taarifa za ufuatiliaji zinaonesha kwamba mikopo iliyotolewa imesaidia kupanua shughuli za kilimo na pia imeongeza kipato cha wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogowadogo *(SELF)*, uliidhinisha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 iliyonufaisha

wajasiriamali 2,071. Hali ya urejeshaji wa mikopo ni wastani wa asilimia 93.4. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa watendaji wa asasi ndogo 123 za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja ilikuwa dola za Kimarekani 650 milioni ikilinganishwa na dola 744 milioni mwaka 2008, sawa na upungufu wa asilimia 14.5. Hii ilitokana na athari zilizotokana na msukosuko wa masoko ya fedha na mitaji.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vipaumbele katika muda wa kati kuanzia mwaka 2010/2011, Serikali imebainisha maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa kwa kuwekeza katika shughuli za kiuchumi na kijamii zinazoweza kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi kwa upana zaidi. Maeneo hayo ni kilimo, maendeleo ya mifugo na uvuvi; miundombinu; maendeleo ya ardhi na makazi; nishati; viwanda na vitambulisho vya kitaifa. Sekta za kijamii (elimu, afya na maji) zitaendelea kupewa umuhimu katika mgao wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele yaliyotajwa hapo juu, yataendelea kutekelezwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo ya Milenia; MKUKUTA II na Utekelezaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti. Maeneo yaliyobainishwa na sekta husika kama vipaumbele ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kilimo, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea na utekelezaji wa programu mbalimbali za uendelezaji kilimo, mifugo na uvuvi kama ilivyoainishwa katika mipango na mikakati mbalimbali ya sekta hizo. Pamoja na hilo, kipaumbele kimewekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza na kusaidia sekta ndogo ya mazao;

(ii) Kuendeleza na kusaidia sekta ndogo ya mifugo;

(iii) Kuendeleza miundombinu ya maji na ya umwagiliaji; na

(iv) Kuendeleza uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali katika kuboresha miundombinu nchini ili kuongeza ukuaji wa uchumi na kuvutia wawekezaji. Katika kipindi cha muda wa kati, kipaumbele katika uendelezaji wa miundombinu kitakuwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuelekeza rasilimali zaidi katika kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji, hususan ujenzi na ukarabati wa barabara na reli na kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam;

(ii) Kujenga sehemu za kuhifadhi makasha nchi kavu (*Inland Container Depots*), kwa ajili ya kupunguza msongamano wa makasha katika bandari zetu hasa Dar es Salaam;

(iii) Kujenga bandari mpya, kukarabati zilizopo na kuzipandisha daraja baadhi ya bandari hizo ili kuweza kuhudumia mizigo ya ndani na ya nje; na

(iv) Kukarabati viwanja vya ndege, ili kuifanya Tanzania kuwa kituo na sehemu muhimu ya biashara ya usafirishaji wa anga kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Ardhi na Makazi, ardhi ni eneo muhimu kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi. Katika kipindi cha muda wa kati, maeneo yatakayopewa kipaumbele katika uendelezaji wa ardhi ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha na kupanua mfumo wa Kitaifa wa taarifa za ardhi ili kuboresha usimamizi wa ardhi;

(ii) Kuanzisha vituo vya Kitaifa vitakavyosaidia upimaji wa ardhi na uchoraji ramani;

(iii) Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika miji ili kukabiliana na changamoto za ukuaji wa miji nchini;

(iv) Utekelezaji wa mipango ya Kitaifa ya matumizi bora ya ardhi, ikijumuisha Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi katika Wilaya na programu nyinginezo; na

(v) Kuanzishwa kwa mikopo ya nyumba kupitia Kampuni ya Mikopo ya Nyumba (Tanzania *Mortgage Refinance Company – TMRC).*

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Kitaifa, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kujenga miundombinu ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu katika utayarishaji wa Vitambulisho vya Taifa ikiwa ni pamoja na mfumo wa ukusanyaji wa takwimu/taarifa za kuzaliwa, vifo na ndoa; na

(ii) Kuanzisha mfumo wa ushirikiano na vyombo vinavyohusika na utayarishaji na utoaji wa nyaraka mbalimbali kama vile Hati za Kusafiria, Leseni za Udereva, Visa na Namba ya Utambulisho ya Mlipa Kodi *(TIN). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nishati, upatikanaji wa nishati ya uhakika ni muhimu sana katika kukuza na kuendeleza uchumi. Nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na matatizo sugu ya uhaba wa nishati na kwa ajili hiyo, Serikali inakusudia kuwekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa umeme;

(ii) Kuendeleza upatikanaji na utumiaji wa umeme wa gesi asilia;

(iii) Kuendeleza miradi ya umeme vijijini kwa kutumia Wakala wa Nishati Vijijini; na

(iv) Kuimarisha, kuboresha na kupanua Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Viwanda, katika muda wa kati, Serikali inakusudia kuwekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza viwanda vitakavyotumia rasilimali za ndani;

(ii) Kuendeleza viwanda mama ikiwa ni pamoja na Mradi wa Chuma Liganga na Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma; na

(iii) Kuendeleza Kanda Maalumu za Uzalishaji *(Special Economic Zones)* na za Uzalishaji wa Bidhaa kwa ajili ya Kuuza Nje *(Export Processing Zones).*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Fedha, Serikali imefanya yafuatayo:-

(i) Kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo;
(ii) Kuimarisha Benki ya Rasilimali Tanzania na Benki ya Wanawake; *(Makofi)*
(iii) Kuharakisha utekelezaji wa kutoa huduma ya kukodisha zana za kilimo na ujenzi *(financial leasing);* na

(iv) Kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya fedha ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi juu ya uwekaji akiba katika mabenki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Misingi na Malengo ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii 2010/2011 – 2012/2013. Misingi ya Uchumi Jumla katika kipindi cha muda wa kati itazingatia yafuatayo:-

(i) Mwenendo wa uchumi wa dunia na hitajio la kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za msukosuko katika uchumi wa dunia;

(ii) Kuendelea kutengamaza vigezo muhimu vya uchumi jumla na maendeleo ya jamii, hususan mfumuko wa bei;

(iii) Kutekeleza miradi ya kipaumbele kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2010/2011 – 2012/2013;

(iv) Kuweka msukumo katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo, MKUKUTA II na kuelekeza rasilimali kwenye maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kwa haraka zaidi;

(v) Kuweka msukumo katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza, ili kuleta mageuzi endelevu ya kijamii;

(vi) Kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara na kuinua ukuaji wa sekta binafsi;

(vii) Kuimarisha sera za fedha zitakazowiana na mfumo wa sera za mapato na matumizi, zitakazowezesha kuwa na kiwango cha chini cha mfumuko wa bei na pia kuwa na tofauti ndogo kati ya riba za amana na mikopo ya benki na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi;

(viii) Kuongeza mapato ya ndani;

(ix) Kuendelea kuwepo kwa utulivu wa kisiasa; na

(x) Kuimarisha mfumo wa uratibu na kufanya tathmini, ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi mzuri wa rasilimali za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Uchumi Jumla na Maendeleo y a J a m i i k a t i k a k i p i n d i c h a m w a k a 2010/2011 – 2012/2013, kama ilivyotarajiwa, athari za msukosuko wa uchumi duniani zilikuwa za mpito na hivyo, ukuaji wa Pato la Taifa unakadiriwa kuanza kuongezeka mwaka 2010. Utekelezaji wa sera zilizoainishwa hapo juu unalenga kufikia malengo yafuatayo katika kipindi cha mwaka 2010/2011 - 2012/2013;

(i) Pato halisi la Taifa litakua kwa asilimia 7.0 mwaka 2010, asilimia 7.1 mwaka 2011, asilimia 7.4 mwaka 2012, na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 7.8 ifikapo mwaka 2013;

(ii) Kasi ya upandaji bei inakisiwa kupungua kufikia asilimia 8.0, ifikapo mwishoni mwa Juni 2010 na kupungua zaidi hadi asilimia 5.0 ifikapo Juni 2011;

(iii) Kuongezeka kwa mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa kwa asilimia 17.3 mwaka 2010/2011, asilimia 17.4 mwaka 2011/2012 na asilimia 17.6 mwaka 2012/2013;

(iv) Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) na pana zaidi (M3) katika wigo wa asilimia 20.0 kwa zote mbili, mwishoni mwa Juni 2010, utakaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma toka nje kwa kipindi kisichopungua miezi mitano;

(vi) Kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara;

(vii) Kuweka msukumo zaidi katika kuendeleza kilimo na kuwa na usalama wa chakula;

(viii) Kupunguza tofauti ya viwango vya riba; na

(ix) Kuwa na kiwango imara cha ubadilishaji wa fedha kitakachotokana na mwenendo wa soko la fedha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza Hali ya Uchumi wa Taifa, changamoto, misingi na malengo ya mpango na bajeti kwa kipindi cha 2010/2011 – 2012/2013, ni wazi kwamba hatua zilizochukuliwa na Serikali kukabiliana na athari za kuyumba kwa uchumi wa dunia, kwa kiasi kikubwa, zimeweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Juhudi zitaendelea kuelekezwa katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi unaimarika.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza mambo muhimu ambayo tunahitaji kuyapa msukumo zaidi katika utekelezaji na ufuatiliaji wa karibu kwa mwaka 2010/2011 kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza msukumo katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025;

(ii) Kuendelea kuimarisha uchumi na kukuza Pato la Taifa ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za msukosuko wa kiuchumi;

(iii) Kuongeza uwekezaji katika maeneo ya vipaumbele na yenye mwingiliano kisekta, hususan kilimo, miundombinu, viwanda, ardhi na nishati, kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na ya kufanya biashara na kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika maeneo hayo;

(iv) Kuhimiza na kuhamasisha utekelezaji wa Kilimo Kwanza;

(v) Kusimamia utekelezaji wa Awamu ya Pili ya MKUKUTA;

(vi) Kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi baina ya Tanzania na nchi nyingine;

(vii) Kuimarisha usimamizi katika matumizi ya fedha za umma;

(viii) Kuongeza ajira; na

(ix) Kuendeleza ukanda mpya wa kilimo ambao wawekezaji wadogo, wakubwa, Serikali na wadau wengine wa maendeleo watagawana majukumu, kuhakikisha kunakuwepo na maendeleo, hivyo kuleta tija katika sekta ya kilimo. Ukanda huo ni eneo lililounganishwa na Reli ya Uhuru (TAZARA) na pia Mikoa ya Pwani, Morogoro, Mbeya na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kuwa, hivi sasa uchumi wetu unakumbana na changamoto nyingi kutokana na athari zilizojitokeza za kuyumba kwa uchumi wa dunia. Tunalazimika kuchukua hatua za dhati katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi;

(ii) Kuzalisha chakula cha kutosha kwa mahitaji yetu na kuwa na akiba ya kuridhisha;

(iii) Kuongeza mapato ya ndani pamoja na kudhibiti matumizi ili tuweze kugharamia matumizi ya kawaida kwa fedha zetu wenyewe kwa kiwango kikubwa zaidi kila mwaka; *(Makofi)*

(iv) Kuendelea kuweka msukumo zaidi katika kukuza mauzo nje ya bidhaa na huduma, kama mbinu muhimu ya kujenga uwezo wetu wa kujitegemea;

(v) Kutumia fursa ya nchi yetu kuwa kiungo muhimu kibiashara na nchi zinazotuzunguka, ambazo hazina bandari; na *(Makofi)*

(vi) Kujizatiti katika kuboresha mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa maana ya kuwasilisha taarifa ya hali ya uchumi kwa nchi yetu imewasilishwa na imeungwa mkono. Lakini kama ilivyokawaida, hoja hii huwa inaamuliwa kwa pamoja na hoja atakayoitoa leo saa kumi, zinazungumzwa kwa pamoja na kwa safari hii kwa muda wa siku tatu baada ya hapo ndiyo tutaweza kuiamua. Kwa kuwa sasa shughuli za asubuhi hii ndiyo tumefikia tamati, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi leo jioni. *(Makofi)*

*(Saa 5.16 asubuhi Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, vipo vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina takwimu mbalimbali za Bajeti. Kitabu cha Kwanza kinahusu Makisio ya Mapato. Kitabu cha Pili na cha Tatu, ni vya Makisio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kitabu cha Nne, kinaelezea makadirio ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2010 ambao ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii kueleza kuwa, Bajeti ya mwaka wa fedha 2009/2010 unaomalizika mwezi huu, inakamilisha kipindi cha miaka mitano cha Serikali ya Awamu ya Nne iliyoingia madarakani Desemba 2005. Katika kipindi hiki, Bajeti imetumika kama chombo muhimu katika kutekeleza Sera na Malengo ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala cha CCM. Kwa hiyo, bajeti ya mwaka wa fedha 2010/2011, inalenga kuendelea na utekelezaji wa sera na malengo ya kiuchumi na kijamii. Katika kipindi hiki, yamekuwepo mafanikio ya kuridhisha katika kutoa huduma bora kwa wananchi na kuimarisha miundombinu ili kuwezesha uchumi kukua na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha matayarisho ya Bajeti hii. Maandalizi ya bajeti ya Serikali yanahusisha wadau na vyombo mbalimbali. Kipekee, ninaishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni, pamoja na Kamati nyingine za kisekta, kwa ushauri mzuri waliotoa wakati wakichambua mapendekezo ya bajeti hii. Naomba niishukuru kwa namna ya pekee, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2010 na nyaraka mbalimbali za kisheria ambazo ni sehemu ya bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Fedha na Uchumi, nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Jeremiah H. Sumari (Mb) na Mheshimiwa Omari Y. Mzee (Mb). Namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhani M. Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu, Ndugu John M. Haule, Ndugu Laston T. Msongole na Dkt. Servacius B. Likwelile, pamoja na Katibu Mtendaji Tume ya Mipango, Dkt. Philip. I. Mpango. Aidha, napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Vile vile, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha hotuba hii kwa wakati. Mwisho, nawashukuru wataalamu na wale wote waliotoa mapendekezo kuhusu sera, mikakati na masuala mbalimbali ya kodi ambayo yamezingatiwa katika kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, huu ni mkutano wa mwisho wa Bajeti kwa Bunge hili baada ya miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Wengi wetu tutarudi

kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi yetu, kuomba ridhaa yao ya kurudi tena katika ukumbi huu. Nina matumaini makubwa kuwa, wananchi hawatasahau kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Awamu hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA); Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs); na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Napenda kulipongeza Bunge lako Tukufu chini ya uongozi wako, kwa mchango mkubwa ambao umeiwezesha Serikali kupata mafanikio makubwa katika kipindi hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha Awamu ya Nne. Yafuatayo ni baadhi ya mafanikio ya Serikali katika kipindi cha kwanza cha Awamu ya nne:-

(i) Mapato ya ndani ya Serikali yameongezeka kwa asilimia 121 kutoka shilingi 2,124.8 bilioni mwaka 2005/06 hadi shilingi 4,688.3 bilioni ambazo zinatarajiwa kukusanywa kwa mwaka 2009/10. Mapato ya ndani yamefikia zaidi ya wastani wa shilingi 390 bilioni kwa mwezi ikilinganishwa na wastani wa shilingi 177 bilioni mwaka 2005/2006, sawa na ongezeko la zaidi ya mara mbili katika kipindi hicho. Aidha, mapato ya ndani kama asilimia ya Pato la Taifa yaliongezeka kutoka asilimia 12.5 mwaka 2005/06 hadi asilimia 16.4 mwaka 2009/10. Hii imesababishwa na jitihada za Serikali katika kuboresha sera za kodi na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato;

(ii) Jumla ya misaada na mikopo ya Bajeti *(GBS)* iliongezeka kutoka shilingi 588.702 bilioni mwaka 2005/2006 hadi shilingi 1,307.707 bilioni zinazotarajiwa kupatikana kwa mwaka 2009/2010. Aidha, misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo iliongezeka kutoka shilingi 1,047.266 bilioni mwaka 2005/06 hadi kufikia shilingi 2,825.431 bilioni ambazo zinatarajiwa kupatikana kwa mwaka 2009/2010. Hii imetokana hasa na utekelezaji wa Mkakati wa Pamoja wa kusimamia Misaada (MPAMITA) pamoja na uhusiano mzuri uliopo baina yetu na washirika wa maendeleo;

(iii) Jumla ya matumizi ya Serikali yaliongezeka kutoka shilingi 4,131.946 bilioni mwaka 2005/2006 na matarajio ni kwamba hadi Juni 2010 matumizi yote yatakuwa shilingi 9,238.801 bilioni. Katika kipindi hicho matumizi yalizingatia katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, MKUKUTA, Malengo ya Milenia 2015 na katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005;

(iv) Mikopo iliyotolewa na mabenki kwa sekta binafsi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi iliongezeka kutoka shilingi 1,571.0 bilioni mwezi Desemba 2005 hadi shilingi 4,836.0 bilioni mwezi Oktoba 2009. Sera sahihi za fedha (*prudent monetary policy*) zimechangia ongezeko hilo;

(v) Deni la Taifa limepungua kutoka Dola za Kimarekani 10.01 bilioni mwaka 2005/2006 hadi kufikia Dola za Kimarekani 8.25 bilioni mwaka 2008/2009 sawa

na upungufu wa asilimia 18. Kwa mujibu wa mwenendo wa viwango vya deni kuwa himilivu, Deni la Taifa linaonesha kuwa linadhibitiwa na linahimilika;

(vi) Miundombinu ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na barabara, nishati na umwagiliaji imejengwa na kukarabatiwa. Sekta ya elimu imeimarishwa ikiwa ni pamoja na kujenga shule za sekondari za Kata, Chuo Kikuu cha Dodoma na kuvipa hadhi baadhi ya vyuo kuwa vyuo vikuu;

(vii) Mfuko wa Uwezeshaji Kiuchumi umeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kutoa Shilingi 10.5 bilioni katika awamu ya kwanza kupitia mabenki ya *CRDB* na *NMB*. Fedha hizo ziliongezwa mara tatu na kufikia shilingi 31.5 bilioni. Aidha, hadi Desemba, 2009 jumla ya wajasiriamali 66,559 walikuwa wamefaidika na mikopo iliyotolewa ikiwa na uwiano wa wanaume 42,851 na wanawake 23,708. Kadhalika, katika awamu ya pili, Serikali imetoa Shilingi 10.5 bilioni; kati ya hizo Shilingi 600 milioni zilipelekwa Zanzibar na Shilingi 9.9 bilioni Tanzania Bara; Vile vile Serikali inatambua na kuthamini mchango wa taasisi zisizo za kiserikali katika kuwawezesha wananchi kama vile *FINCA*, *Presidential Trust Fund (PTF)*, *PRIDE*, VICOBA na kadhalika;

(viii) Mfuko wa Uwezeshaji wa Wajasiriamali Wadogo (*Small Enterpreneurs Loan Facility-SELF*), umeendelea kutoa mikopo katika kipindi cha Awamu ya Nne. Mwaka 2005 ilitoa mikopo ya shilingi 5.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2010, jumla ya mikopo iliyotolewa ilikuwa shilingi 25.1 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 348. Vile vile, taasisi za fedha zilizofaidika na mikopo ya *SELF* ziliongezeka kutoka 175 mwaka 2005 hadi 247 Machi 2010 sawa na ongezeko la taasisi 72. Idadi ya wanufaika iliongezeka toka 20,526 mwaka 2005 hadi 69,795 mwaka 2010. Kati ya hao wanawake ni asilimia 58;

(ix) Mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ulianzishwa mwaka 2007 kwa mtaji wa shilingi 400 milioni. Mfuko huo umeendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali, ambapo hadi Desemba 2009, mikopo yenye thamani ya shilingi 4.2 bilioni ilitolewa kwa wajasiriamali 4,437 wakiwemo wanawake 1,341 na wanaume 3,096; na

(x) Mfuko wa Udhamini wa mikopo kwa ajili ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi (ECGS) na Mfuko wa Udhamini wa wafanyabiashara wadogo na wa kati *(SME's-CGS)* imeongeza mitaji kutoka shilingi 500 milioni Septemba mwaka 2005 hadi shilingi 5.751 bilioni mwezi Machi mwaka 2010. Hii imeongeza wigo wa ukopeshaji kwa wafanyabiashara kupitia mabenki husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio niliyoainisha, bado kuna changamoto mbalimbali za kibajeti kama ifuatavyo:-

(i) Mapato ya ndani hayawiani na mahitaji ya kugharamia shughuli mbalimbali za Serikali, hususan miradi ya miundombinu ya reli, barabara, bandari, viwanja vya ndege na umwagiliaji; huduma za jamii (elimu, afya na maji); na kilimo;

(ii) Sehemu kubwa ya shughuli zinazohusiana na uchumi wetu kutoingizwa katika sekta rasmi na hivyo kuendelea kuwa na mchango mdogo katika mapato ya ndani;

(iii) Kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na uelewa mdogo wa Sheria ya Manunuzi ya Umma 2004, kuchelewa kupatikana kwa fedha za maendeleo; na

(iv) Utumiaji wa mfumo wa kutayarisha na kutoa taarifa za hesabu *(IFMS)* haujasambaa kikamilifu kufikia Halmashauri zote hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya Hali ya Uchumi niliyowasilisha leo asubuhi, nilieleza mwenendo wa uchumi wa nchi tokea mwaka 2005/2006 mwanzo wa Awamu ya Nne hadi mwaka 2009 na malengo ya uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2010/2011 – 2012/13). Napenda sasa kuchukua fursa hii kutoa maelezo kuhusu mapitio ya Bajeti ya mwaka 2009/2010 katika kipindi cha miezi tisa ya kwanza ya mwaka huu; Mwelekeo wa Bajeti hadi Juni 2010 na Misingi na Shabaha ya Bajeti kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Sera za Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Sera za Bajeti kwa 2009/2010, zilihusisha sera za mapato ya ndani; matumizi; misaada na mikopo. Sera za Mapato zilihusisha hatua za kupanua wigo wa mapato; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali; kuchukua hatua za kupunguza misamaha ya kodi na kuweka vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, sera za matumizi zililenga kutoa upendeleo wa mgao wa matumizi kwenye sekta za kipaumbele ikiwa ni pamoja na elimu, miundombinu na kilimo. Aidha, Sera za matumizi pia zilihusisha kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa matumizi pamoja na tathmini ya mpango na bajeti ili kuhakikisha rasilimali fedha inatumika kwa ufanisi. Hatua za kibajeti zilichukuliwa kukabiliana na athari zinazotokana na msukosuko wa kiuchumi duniani; kutenga fedha za kugharamia miradi maalum katika maeneo yenye mazingira yasiyovutia watumishi kufanya kazi; kuboresha utoaji wa huduma na kuendeleza mafanikio yaliyopatikana katika programu muhimu za kijamii kama vile afya, elimu na maji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa misaada na mikopo, Serikali ilidhamiria kutafuta misaada na mikopo yenye masharti nafuu na yenye manufaa ili kuweza kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu ikiwa ni pamoja na kushirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sera hizo, Serikali ilipanga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 9,513.685 bilioni kutokana na mapato ya ndani, mapato kutoka Serikali za Mitaa, misaada na mikopo ya nje, mikopo ya ndani na mapato ya ubinafsishaji. Aidha, Serikali ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 9,513.685 bilioni sawa na mapato yote. Hata hivyo, kufuatia Bajeti ya nyongeza iliyopitishwa na Bunge mwezi

Februari 2010, Mapato na Matumizi yaliongezeka kwa kiasi cha shilingi 19.0 bilioni na hivyo kufikia shilingi 9,532.685 bilioni kutokana na mapato mapya.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/10 yalikuwa ni kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi 5,096.016 bilioni sawa na asilimia 16.4 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15.9 mwaka 2008/09. Ili kuhakikisha kuwa jukumu la kukusanya mapato hayo linatekelezwa kwa ufanisi kama ilivyopangwa, hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kupanua wigo wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi na kuendelea kuimarisha uchumi tulivu pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua;

(ii) Kusimamia kwa karibu mageuzi yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* chini ya Mpango wake wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano (*Third Corporate Plan*) ambao malengo yake ni pamoja na: kuziba mianya ya ukwepaji kodi; kudhibiti uvujaji wa mapato ya Serikali; kuendelea kutoa elimu ya biashara; na kuimarisha namna ya ukokotoaji kodi kwa wafanyabiashara;

(iii) Kuendelea kurekebisha mfumo wa kodi na kuimarisha Idara ya Walipakodi Wakubwa kwa kuboresha mifumo ya utendaji;

(iv) Kuendelea kuboresha usimamizi na utendaji katika Idara ya Forodha kwa kuongeza uwajibikaji, matumizi ya teknolojia na kupunguza kero kwa walipa kodi;

(v) Kuendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti katika kupeleka mizigo kwenye bandari za nchi kavu (*Inland Container Depot - ICD*), ikiwemo matumizi ya teknolojia ya kisasa;

(vi) Kuimarisha udhibiti wa bidhaa za mafuta ya petroli, ikiwemo kuhakikisha kuwa, mita za kupitishia bidhaa hizo (*flow metres*) zinafanya kazi kwa ufanisi wakati wote;

(vii) Kuhakikisha kuwa mafuta yanayopitishwa hapa nchini kwenda nchi jirani (*transit goods*) hayauzwi katika soko la ndani;

(viii) Kushirikiana na Mamlaka husika ili kudhibiti uchanganyaji wa dizeli na mafuta ya taa kwa lengo la kudhibiti uvujaji wa mapato na kuhakikisha ubora na usalama wa vyombo vinavyotumia dizeli;

(ix) Kuanzisha na kuendesha ghala la forodha kwa ajili ya bidhaa za mafuta (*TIPER Fuel Bonded Warehouse*). Hatua hii itawezesha kuwa na hifadhi ya mafuta, kudhibiti mapato ya Serikali pamoja na kuongeza ufanisi wa soko la bidhaa za mafuta kwa kupunguza gharama za uagizaji na uendeshaji na hivyo kuweza kushusha bei kwa watumiaji;

(x) Kuboresha ukaguzi wa kodi (*field and desk audits*) na usimamizi wa ukusanyaji wa malimbikizo ya kodi;

(xi) Kuboresha usimamizi wa mapato ya kodi ya majengo na mapato ya kodi yatokanayo na ukodishaji au upangishaji wa majengo hayo; na

(xii) Kukamilisha tathmini ya utaratibu na utambuzi wa vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea kwa lengo la kubaini upungufu uliopo na kufanya marekebisho ili kuongeza ufanisi na udhibiti wa makusanyo ya mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani sura 148. Marekebisho hayo yalijumuisha kupunguza kiwango kilichokuwa kikitozwa awali cha asilimia 20 ya mauzo hadi asilimia 18 ili kujenga mazingira ya kuongeza kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari, kuanza kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye muda wa maongezi kwenye simu kwa kutumia bei halisi inayooneshwa kwenye vocha badala ya bei nafuu anayotozwa muuzaji wa jumla, na kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upangishaji na ukodishaji wa nyumba na majengo.

Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilitoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye matanki maalum ya kuhifadhi maziwa na vipipa vya alumini vinavyotumika kukusanya maziwa kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya vyombo hivyo ili kuongeza ubora wa maziwa na kipato kwa wafugaji. Vile vile, Serikali ilianza kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za upakiaji na upakuaji mizigo kwenye meli za mizigo zinazotoka nje ya nchi; pamoja na kutoa msamaha wa kodi hiyo kwenye huduma za kilimo za kutayarisha mashamba, kulima, kupanda na kuvuna ili kupunguza gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2009/2010, Serikali pia ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa sura 147, kwa kutoza ushuru wa bidhaa katika huduma za simu za mkononi pale vocha ama muda wa maongezi unapouzwa badala ya kusubiri hadi muda wa maongezi utumike.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia matakwa ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mawaziri wa Fedha wa Nchi wanachama waliridhia kufanya marekebisho mbalimbali katika Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kama ilivyoainishwa kwenye Hotuba yangu ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 hadi Machi, 2010, Serikali ilikusanya mapato ya ndani kiasi cha Sh. 3,490,263,000/= sawa na asilimia 91.3 ya lengo la kukusanya Sh. 3,821,397,000/=. Mwenendo huu unaonesha upungufu wa shilingi bilioni 331.133 ikilinganishwa na lengo. Upungufu ulijitokeza kwenye ushuru wa bidhaa kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa kodi hii hasa sigara, bia na vinywaji baridi. Aidha, upungufu katika mapato yasiyo ya kodi ulijitokeza kwenye ada na tozo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mapato kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mauzo ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 564.798, ikiwa ni asilimia 90 ya makadirio. Mapato kutokana na kodi hiyo kwa uagizaji kutoka nje yalifikia shilingi bilioni 568.984 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 556.643, ikiwa ni asilimia mbili juu ya lengo. Kwa uagizaji kutoka nje, makusanyo halisi ya Ushuru wa Forodha yalikuwa shilingi bilioni 282.309, sawa na asilimia 90 ya malengo ya kukusanya shilingi bilioni 314.251.

Aidha, mapato kutokana na ushuru wa bidhaa zinazozalishwa nchini yalifikia shilingi bilioni 230.846, sawa na asilimia 83 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 278.617, wakati shilingi bilioni 393.555 zilikusanywa kutokana na ushuru wa bidhaa zilizoagizwa nje ikilinganishwa na shilingi bilioni 448.660 zilizokadiriwa, sawa na upungufu wa asilimia 12. Makusanyo halisi yanayotokana na vyanzo vya kodi ya mapato yalikuwa shilingi bilioni 1,039.887, ikiwa ni asilimia 94 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,108.908.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara, Idara na Mikoa yalifikia shilingi bilioni 160.243, sawa na asilimia 80 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 199.653. Upungufu huu unatokana na sababu zilizoelezwa hapo awali. Kwa upande mwingine, kufikia Machi, 2010 kiasi cha shilingi bilioni 9.659 zilipatikana kutokana na uuzaji wa baadhi ya hisa za Serikali *NMB* ambapo lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ni shilingi bilioni 15.0. Taratibu zinaendelea ili kuuza bakaa ya hisa hizo kwenye soko la Hisa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 506.193, sawa na asilimia 1.6 ya pato la Taifa kutoka vyanzo vya ndani ikiwa ni moja ya hatua za kukabiliana na msukosuko wa uchumi duniani. Hadi Machi, 2010, kiasi cha shilingi bilioni 155.3 kilikopwa kwa ajili hiyo. Aidha, dhamana za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 424.393 ziliuzwa katika soko ili kulipia zilizoiva *(roll-over)* na kusaidia kudhibiti ujazi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2009 – Machi, 2010, jumla ya misaada na mikopo ya bajeti *(GBS)* iliyopokelewa ilikuwa shilingi bilioni 998.676 sawa na asilimia 84 ya shilingi bilioni 1,193.91 zilizokadiriwa kwenye bajeti. Misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo (ikijumuisha Mfuko wa *Basket*) ilifikia shilingi bilioni 1,380.883, sawa na asilimia 93 ya makadirio katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwianisha matumizi yake na sera za utekelezaji wa MKUKUTA ikiwa ni nguzo muhimu ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025. Aidha, bajeti ya mwaka 2009/2010 ilielekeza rasilimali zaidi katika elimu, miundombinu, kilimo na afya. Katika kipindi cha Julai, 2009 - Machi 2010, matumizi halisi yalikuwa shilingi bilioni 6,143.918 sawa na asilimia 91 ya makadirio ya shilingi bilioni 6,718.713. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4,189.721 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1,954.197 ni matumizi ya maendeleo. Matumizi haya yamegharamiwa na mapato ya ndani, misaada ya nje, mikopo ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali kwa kipindi cha Julai, 2009 – Machi, 2010 yalikuwa shilingi bilioni 1,276.706 sawa na asilimia 97 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,320.908. Malipo ya riba kwa madeni ya ndani yalifikia shilingi bilioni 145.914, sawa na asilimia 62 ya lengo la kulipa shilingi bilioni 236.638 na kiasi cha shilingi bilioni 27.681 kilitumika kulipia riba kwa madeni ya nje, sawa na asilimia 73 ya makadirio. Kwa upande wa matumizi ya madeni mengine *(CFS Others),* jumla ya shilingi bilioni 276.569 zilitumika, ikiwa ni asilimia 81 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, matumizi mengine katika Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 2,462.851 sawa na asilimia 97 ikilinganishwa na makadirio kwa kipindi hicho. Mwenendo wa matumizi umekwenda sambamba na upatikanaji wa mapato katika kipindi hicho. Aidha, matumizi ya maendeleo yalifikia jumla ya shilingi bilioni 1,954.197 zikijumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 625.383 na shilingi bilioni 1,328.814 fedha za nje, ikiwa ni asilimia 75 na asilimia 93 ya makadirio kwa mtiririko huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali Kuu imeendelea kujenga mazingira wezeshi katika Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuzipatia fedha, watumishi, vitendea kazi na ushauri wa kitaalamu kulingana na maeneo yaliyoainishwa kwenye Bajeti. Hadi kufikia Machi, 2010, Serikali za Mitaa zilikuwa zimepokea jumla ya shilingi bilioni 1,348.370 sawa na asilimia 65.9 ya lengo la shilingi bilioni 2,044.567 zilizoidhinishwa na Bunge. Kwa upande wa watumishi, Serikali imeweza kuajiri jumla ya watumishi 394 na kati ya hawa, wahasibu ni 307 na Wakaguzi wa Ndani 87 ambao wameongeza uwezo wa Halmashauri katika kutekeleza bajeti ya Serikali.

Aidha, wakuu wa Idara za Halmashauri wapatao 800 walipatiwa mafunzo ya kina juu ya uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za bajeti ili kuongeza uwezo wa kusimamia bajeti katika maeneo yao ya utawala.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya ndani, Serikali za Mitaa zimeendelea kukusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa sura 290. Katika mwaka wa fedha 2009/2010, mapato kutoka Halmashauri yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 138.052. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010, mapato halisi yaliyokusanywa kwenye Halmashauri yalifikia jumla ya shilingi bilioni 86.263 sawa na asilimia 62.5 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha nyingi kwenye Halmashauri nchini kupitia idadi kubwa ya Akaunti zilizofunguliwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Hali hii imesababisha kuwepo kwa akaunti nyingi bila ulazima, kuchanganya fedha katika akaunti zisizostahili, kuongeza mzigo wa kazi za wataalamu katika kufunga hesabu za kila akaunti, na kuongeza gharama za uendeshaji wa akaunti nyingi zisizotumika. Ili kuimarisha usimamizi wa fedha Serikali itaendelea kupunguza Akaunti katika ngazi za Halmashauri kwa lengo la kubakiza akaunti chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, baadhi ya Halmashauri zimekuwa na matumizi ya fedha yasiyoridhisha hali inayosababisha kupata hati zenye mashaka au hati chafu. Aidha, fedha nyingi zinazotumwa kwenye Halmashauri, hususan fedha za Maendeleo, zimekuwa zikilundikana kwenye Akaunti bila kutumika kwa wakati na hivyo kuwakosesha wananchi huduma bora katika muda uliokusudiwa. Hatua zitachukuliwa kurekebisha hali hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutumia teknolojia ya kisasa katika mfumo wa bajeti na uhasibu ujulikanao kama "*Integrated Financial Management System (IFMS)*". Katika Mfumo huo, jumla ya Halmashauri 87 zimeunganishwa kwenye mtandao wa bajeti ya matumizi *(Epicor System)* na hatua zinaendelea kuunganisha Halmashauri zilizosalia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, Serikali imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo unaotekelezwa kwa kuzingatia Sheria Na. 6 ya mwaka 2009. Serikali imekamilisha kutoa fedha za Mfuko huo ambazo zitaongeza chachu ya kuchangia miradi mbalimbali ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa fedha zote zinazopelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza shughuli zilizokusudiwa, Serikali imeendelea kujenga uwezo wa Idara za Mipango, Uhasibu, pamoja na Ukaguzi wa Ndani. Idara hizi kwa ujumla ndizo husimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri na kuhakikisha bajeti inaleta manufaa kwa walengwa kulingana na makusudio ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2008/2009 imeonesha kuimarika kwa udhibiti na usimamizi wa Fedha za umma katika Wizara na Idara za Serikali Kuu na kupungua kwa hoja za ukaguzi wa fedha za umma. Taarifa imeonesha kuongezeka kwa Hati Safi za Ukaguzi zilizotolewa kwa Wizara na Idara za Serikali Kuu kutoka asilimia 70 kwa hesabu za mwaka 2007/2008 na kufikia asilimia 86 mwaka 2008/2009. Napenda kupongeza Wizara na Idara hizo zilizopata hati safi katika mwaka huo. Pamoja na kuimarika kwa usimamizi wa fedha za umma, Serikali inatambua kuwa bado upo udhaifu wa usimamizi wa fedha za umma katika Serikali za Mitaa. Kutoimarika kwa usimamizi wa matumizi katika Serikali za Mitaa kumejionesha pia katika taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC).*

Mheshimiwa Spika, kadhalika, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2008/2009 inaonesha udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma katika maeneo yafuatayo:-

- Kutofuatwa kwa usahihi kwa uandaaji wa hesabu katika viwango vya kimataifa *(IPSAS);*

- Kutozingatia sheria na kanuni za ununuzi, mifumo dhaifu ya usimamizi na udhibiti wa mali za Serikali na ukusanyaji wa mapato;

- Udhaifu katika ulipaji wa mishahara; na

- Kutotekelezwa kwa wakati mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali yaliyotolewa kwenye taarifa zake za miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, hatua zinachukuliwa kurekebisha udhaifu huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha maandalizi ya MKUKUTA awamu ya Pili utakaoanza kutekelezwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Maandalizi ya MKUKUTA awamu ya Pili ni matokeo ya tafiti mbalimbali na mijadala ya wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini, Wahisani, vyama vya Wafanyakazi na sekta binafsi. MKUKUTA II utaendelea kujengwa katika misingi ya matokeo tarajiwa katika nguzo kuu tatu (Kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuboresha hali ya maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji). Msisitizo ukiwa katika kukuza na kusimamia uchumi, kuboresha utoaji huduma za jamii, na kuboresha utaratibu wa utekelezaji. Kwa miaka mitano ijayo, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kugharamia MKUKUTA II hasa vipaumbele vichache katika kukuza uchumi wenye kugusa walio wengi, na kuboresha huduma za jamii. Sekta binafsi pia inatarajiwa kuunga mkono juhudi za Serikali kupitia miradi mbalimbali ikiwemo utaratibu wa *Public Private Partinership*s. Vipaumbele viko katika misingi mikuu minne:-

(i) Kuendeleza na kuhakikisha matumizi bora ya njia kuu za uzalishaji ikiwemo rasilimali watu, ardhi na mtaji;

(ii) Kuboresha na kuimarisha taasisi za uchumi;

(iii) Kujenga na kuimarisha miundo mbinu ya uchumi hasa umeme, maji, barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege; na

(iv) Kuimarisha usimamizi wa uchumi ili kujenga uwezo wa Serikali katika kuwezesha sekta binafsi na sekta nyingine kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa kuhusu mwenendo wa bajeti katika kipindi cha miezi tisa hadi Machi, 2010, matarajio ni kwamba hadi Juni, 2010, mapato ya ndani yatafikia shilingi 4,688.335 bilioni (trilioni 4.7) ikiwa ni chini ya lengo la bajeti kwa asilimia nane au shilingi bilioni 407.681. Baadhi ya wahisani wametoa misaada na mikopo zaidi ya kibajeti *(GBS)* kuisaidia Serikali kukabiliana na athari za msukosuko wa kiuchumi. Kufuatia hilo, hadi kufikia Juni, 2010, misaada na mikopo inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 1,307.707 ikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 1,193.91.

Ongezeko hili litasaidia kupunguza pengo lililojitokeza kwenye mapato ya ndani. Kwa upande wa misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo, matarajio ni kwamba fedha zitapatikana kama zilivyopangwa kwenye bajeti. Serikali itaendelea kukopa kutoka soko la ndani kama ilivyopangwa kwenye bajeti ya 2009/2010 ili kugharamia matumizi, pamoja na kulipia dhamana za Serikali zinazoiva (*roll-over*). Kwa upande wa matumizi, Serikali itarekebisha matumizi yake ili kuwianisha na mapato yanayotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa bajeti wa mwaka 2010/11 unazingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA), Malengo ya Maendeleo ya Milenia *(MDGs),* Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Madeni, Vipaumbele vya uwekezaji wa umma kama vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Mpango na Bajeti mwaka 2010/11-2012/13, na Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA). Misingi na shabaha ya bajeti ya Serikali kwa kipindi cha 2010/2011 itakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea kuboresha mfumo wa makusanyo ya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa mapato kwa kuhusisha vyanzo vipya;

(ii) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa makusanyo kutoka vyanzo mbalimbali;

(iii) Kuendelea kuchukua hatua za kudhibiti misamaha ya kodi ili kuongeza mapato;

(iv) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa kaulimbiu ya Kilimo Kwanza;

(v) Kuharakisha zoezi la kuanzishwa kwa vitambulisho vya Taifa;

(vi) Kuongeza rasilimali katika utekelezaji wa MKUKUTA II kwa kupeleka rasilimali za kutosha katika maeneo machache yenye kuongeza kasi ya ukuaji uchumi;

(vii) Kutenga fedha za kuiwezesha sekta ya Ardhi kupima na kutenga maeneo kwa matumizi mbalimbali ya ardhi;

(viii) Kulinda na kudumisha mafanikio yaliyopatikana hadi sasa katika sekta za huduma ya jamii (elimu, afya na maji);

(ix) Kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012;

(x) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji;

(xi) Kuboresha maslahi ya watumishi na kupanua ajira;

(xii) Kuhakikisha Uchaguzi Mkuu unatengewa rasilimali za kutosha ili kuwezesha uchaguzi kufanyika kama ulivyopangwa;

(xiii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje;

(xiv) Kuboresha, kupanua na kukarabati miundombinu ya barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na miradi ya umeme;

(xv) Kuimarisha sera za fedha ili ziendane na zile za mapato na matumizi zitakazosaidia kupunguza mfumuko wa bei, riba na kuongeza mikopo kwa sekta binafsi;

(xvi) Kuzipa uwezo Serikali za Mitaa wa kusimamia rasilimali watu na fedha ili ziweze kutekeleza kwa ufanisi maamuzi ya kupeleka madaraka kwa wananchi; na

(xvii) Kutafuta mikopo zaidi yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nchi na taasisi mbalimbali duniani ili kuongeza uwezo wa Serikali kugharamia miradi mikubwa ya miundombinu ikiwa ni pamoja na kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa ubia *(PPP).*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Sera za mapato zinalenga kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 6,003.59 sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 16.4 kwa mwaka 2009/2010. Kati ya kiwango hicho, shilingi bilioni 5,652.59 ni mapato yatokanayo na kodi na shilingi bilioni 351.0 ni mapato yasiyo ya kodi. Mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 172.582. Aidha, Serikali inategemea kuuza baadhi ya hisa zake katika benki ya *NBC* kupitia soko la Hisa ambapo kiasi cha shilingi bilioni 30 zitapatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza sera za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kuweza kugharamia sehemu kubwa ya matumizi ya kawaida. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha kuwa pale inapowezekana malipo yanafanyika kwenye mabenki;

(ii) Kuweka mkakati wa kuboresha huduma za utalii kwa kutathmini hoteli (*hotel grading*) ili ziwe katika viwango vinavyokubalika kimataifa kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na ada;

(iii)Kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Fedha inayoelekeza mashirika na taasisi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

(iv)Kuendelea kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya na kuimarisha uchumi tulivu pamoja na kuweka mazingira bora ya biashara ili kuwezesha sekta binafsi kukua;

(v) Kuendelea kusimamia kwa karibu mageuzi makubwa yanayoendelea ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania chini ya Mpango wake wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano (*Third Corporate Plan*) ambayo yamekuwa msingi wa kukua kwa mapato ya ndani mwaka hadi mwaka;

(vi)Kuchukua hatua za kuboresha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka Wizara na Idara za Serikali;

(vii) Kupitia upya utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi kwa lengo la kuongeza udhibiti; na

(viii) Kuendelea kuhakikisha kwamba watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanajengewa uwezo kwa kuwapatia utaalam wa kutosha ili kuongeza ufanisi katika ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupokea misaada na mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2010/2011 Serikali inatarajia kupokea shilingi bilioni 821.645 ikiwa ni misaada na mikopo ya kibajeti ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,307.707 zinazotarajiwa mwaka huu wa fedha. Kupungua kwa misaada na mikopo ya kibajeti kunatokana na baadhi ya wafadhili kutoa fedha zilizokuwa zimepangwa kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kutolewa katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 ili kusaidia Serikali kupambana na athari za msukosuko wa kiuchumi duniani kama nilivyoeleza hapo awali. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 2,452.908 zinatarajiwa kupatikana kutokana na misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua washirika wetu wa maendeleo ambao wamekuwa msaada mkubwa katika maendeleo ya nchi. Wahisani hao ni Uingereza, Denmark, Uholanzi, Ubelgiji, Canada, China, Finland, Ufaransa, Ujerumani, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kusini, Kuwait, Norway, Hispania, Sweden, Switzerland, Marekani, India, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *BADEA, European Union, Global Funds,* Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF),* Kuwait *Fund, Nordic Fund, Opec Fund, Saudi Fund*, na Mashirika ya Umoja wa Mataifa. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutumia mikopo nafuu na kuanzia mwaka ujao kuanza kutumia mikopo ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia bajeti yake ya maendeleo. Hata hivyo, kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi ya miundombinu, Katika mwaka 2010/2011, tunatarajia kukopa kutoka soko la ndani na nje kiasi cha shilingi bilioni 1,331.2 ili kukidhi mahitaji makubwa ya kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 797.6 zitakopwa kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zitakazoiva. Serikali itahakikisha kwamba mikopo ya ndani haiathiri utulivu wa hali ya uchumi na kwamba sekta binafsi inapata mikopo kwa riba nafuu ili kuendeleza shughuli zao. Serikali itahakikisha kwamba fedha hizo zinatumika katika miradi ya kipaumbele na yenye tija. Serikali haitakopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida, uamuzi huu unazingatia kwamba Deni la Taifa linaendelea kuhimilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011, Serikali itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uanzishwaji wa *SACCOS* kama njia bora ya kupata mikopo yenye masharti nafuu; kuainisha aina ya mafunzo ya ujasiriamali yanayohitajika kwa lengo la kuendeleza elimu na stadi za ujasiriamali; kutoa mikopo yenye masharti nafuu ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo, hususan vijana na wanawake kuanzisha na kuendeleza miradi inayolenga kuongeza kipato, tija na ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Halmashauri zinategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 172.582 sawa na asilimia 2.9 ya mapato ya ndani yanayokusanywa na Serikali Kuu. Kiasi hiki ni kidogo ikilinganishwa na fursa zilizopo katika mazingira ya Serikali za Mitaa.

Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea kujenga uwezo wa Halmashauri wa kubuni vyanzo vipya vya mapato ikiwa ni pamoja na kuongeza tija katika ukusanyaji wa vyanzo vilivyopo. Serikali itafanya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ili kuongeza wigo wa kukusanya mapato zaidi na kuweka ukomo wa mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo katika miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida.

Aidha, Serikali Kuu itasaidia kutoa mafunzo ya ukadiriaji na ukusanyaji mapato kwa watumishi wanaohusika katika Serikali za Mitaa ili kuwaongezea uwezo zaidi. Ili kuhakikisha kuwa fedha zinazopelekwa kwenye Serikali za Mitaa zinatekeleza shughuli zinazokusudiwa, Serikali itaendelea kuziwezesha na kuziimarisha Idara za Mipango, Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza uwajibikaji, usimamizi na udhibiti wa fedha katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, sera za matumizi ya Serikali zinalenga katika kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma ili kuongeza ufanisi zaidi pamoja na kutoa kipaumbele kwa maeneo muhimu ya kiuchumi yatakayochochea ukuaji wa haraka wa uchumi na kupunguza umaskini, hususan wa kipato. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010, Serikali imetenga fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa, uchaguzi unafanyika kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwepo kwa mipango madhubuti na nidhamu katika usimamizi wa bajeti, hatuna budi kuweka msukumo katika kuimarisha uwianishaji

wa mpango wa muda wa kati na bajeti na kuongeza ufanisi katika matumizi ya rasilimali fedha chache za umma.

Ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Serikali kupitia Tume ya Mipango, itaanza kuandaa Mipango ya Muda wa Kati *(Medium Term Plans-MTPs)* ya miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2010/2011 yanazingatia sera za matumizi zilizoelezwa hapo juu, pamoja na maeneo hayo, Serikali itatoa umuhimu wa kipekee kwa Uchaguzi Mkuu wa Mwezi Oktoba, 2010 ili kuhakikisha kuwa unafanyika kama ulivyopangwa.

Aidha, Serikali itahakikisha mafanikio yaliyokwishapatikana katika sekta za jamii (afya, elimu na maji) yanalindwa. Maeneo mengine ya kipaumbele yatakuwa ni pamoja na Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Viwanda, Maji na Umwagiliaji; Utafiti na maendeleo, Miundombinu ambayo ni barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na nishati; na utekelezaji wa sera ya kupeleka madaraka Serikali za Mitaa *(D by D).* Kwa muhtasari maeneo yatakayohusika ni pamoja na:-

(i) Kuchukua hatua za kukibadilisha kilimo kuwa cha kisasa zaidi na chenye tija kwa kusaidia na kuwezesha uzalishaji wa mbegu bora kwa wingi; kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo; kuboresha mfumo wa utoaji taarifa za masoko kwa wakulima; kujenga miundombinu ya masoko; na kuanzisha na kuimarisha shughuli za uongezaji thamani katika mazao ya kilimo;

(ii) Kuimarisha huduma za ugani na kufanya tafiti juu ya uzalishaji wa mbegu bora za mifugo; na kuboresha utoaji wa ruzuku ya madawa ya mifugo na chanjo;

(iii) Kuimarisha na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ili kufikia azma ya Kilimo Kwanza, ikiwemo kujenga mabwawa ya uvunaji maji ya mvua ili kuongeza wigo wa umwagiliaji;

(iv) Kuongeza upatikanaji wa maji mijini na vijijini;

(v) Kuanzisha vituo vya kitaifa vitakavyosaidia upimaji wa ardhi na uchoraji ramani na utekelezaji wa mipango ya kitaifa ya matumizi bora ya ardhi;

(vi) Kuharakisha utekelezaji wa mradi wa Vitambulisho vya Taifa;

(vii) Kulinda na kudumisha mafanikio katika sekta ya huduma za jamii yaliyopatikana hadi sasa;

(viii) Kuelekeza rasilimali zaidi katika kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji hasa ujenzi na ukarabati wa barabara na reli; kuimarisha miundombinu ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano; na kukarabati viwanja

vya ndege ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu muhimu cha biashara ya usafirishaji wa anga kikanda na kimataifa;

(ix) Kuweka mkazo zaidi katika ufuaji wa nishati ya umeme na kutekeleza miradi mbalimbali kwa kushirikiana na sekta binafsi *(PPP)* ili kuongeza uwezo wa kuzalisha na kusambaza nishati mijini na vijijini;

(x) Kuendeleza wafanyabiashara wadogo na wale wa kati ili waweze kuongeza ubora na thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini kwa kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika mazao, kuwekeza kwenye maghala na maeneo ya viatamizi *(incubator sites);* kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi ya viwanda inayolinda mazingira ikiwa ni pamoja na kuzalisha zana za kilimo; na

(xi) Kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo; kuimarisha Benki ya Rasilimali Tanzania na Benki ya Wanawake na kuharakisha utekelezaji wa kutoa huduma ya kukodisha zana za kilimo na ujenzi (*financial leasing*); na kukamilisha uanzishwaji wa kampuni mahsusi kwa ajili ya kutafuta na kutoa mikopo ya muda mrefu ya nyumba *(Tanzania Mortgage Refinance Company- TMRC).*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele niliyoyaainisha hapo juu, mchanganuo wa bajeti kwa baadhi ya sekta kwa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

(i) Miundombinu imetengewa shilingi bilioni 1,505.1 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,096.6 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 37.3;

(ii) Kilimo kimetengewa shilingi bilioni 903.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 666.9 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 35.5;

(iii) Elimu imetengewa shilingi bilioni 2,045.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,743.9 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 17.2;

(iv) Afya imetengewa shilingi bilioni 1,205.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 963.0 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 25.2;

(v) Maji imetengewa shilingi bilioni 397.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 347.3 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 14.5;

(vi) Nishati na madini imetengewa shilingi bilioni 327.2 ikilinganishwa na shilingi bilioni 285.5 mwaka 2009/2010 sawa na ongezeko la asilimia 14.6; na

(vii) Shilingi bilioni 30 zimetengwa kwa ajili ya utafiti na ufuatiliaji. Maeneo yatakayopata upendeleo katika awamu ya kwanza ni ukarabati wa Miundombinu katika taasisi zinazohusika na tafiti mbalimbali. Katika mwaka huo, Serikali inatarajia kuandaa agenda ya Kitaifa yenye kuonesha maeneo ya kimkakati katika utafiti. Lengo ni kuwa na

maeneo machache ambayo yatatusaidia kupata matokeo katika muda mfupi na kwa kutumia gharama zinazohimilika.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma, Serikali imedhamiria kutekeleza hatua zifuatazo:-

(i) Kudhibiti matumizi ya simu na umeme: Katika eneo hili, Serikali inatumia fedha nyingi kulipa ankara za simu na umeme kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Mikoa na Halmashauri nchini. Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni za Simu na Umeme *(TTCL, TANESCO)* inadhamiria kuanza kutumia mfumo wa malipo kabla ya huduma (kama *LUKU*) kwa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mikoa ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni ya huduma hizo. Hatua hii pia inalenga kuyaimarisha Mashirika haya kimapato; na

(ii) Kudhibiti Matumizi ya Magari: Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali itapunguza idadi ya magari yatakayonunuliwa na itaimarisha Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini *(GPSA)* ili uweze kuratibu ununuzi wa magari ya Serikali, ikiwa ni pamoja na kuainisha aina za magari yatakayonunuliwa kwa lengo la kupunguza gharama za ununuzi, uendeshaji na matengenezo.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zitakazotekelezwa katika mwaka ujao wa fedha ni pamoja na:

(i) Kuhakikisha kwamba, Serikali inalipa posho za nyumba kutokana na uwezo wa bajeti. Posho za nyumba zitatolewa tu kwa wafanyakazi wenye stahili na kwa viwango maalum *(specific rate)* badala ya asilimia ya mshahara kama ilivyo sasa;

(ii) Fedha zilizopangwa kwa ajili ya posho mbalimbali katika Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri zitapunguzwa na kudhibitiwa ili kuepuka matumizi yasiyo ya lazima na ya sio na tija;

(iii) Kuhakikisha kuwa mfumo wa kutayarisha na kutoa taarifa za hesabu *(IFMS)* unasambaa katika Serikali za Mitaa zilizobaki. Lengo ni kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kama zilivyopangwa;

(iv) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani juu ya uandaaji wa hesabu katika viwango vya kimataifa *(IPSAS);*

(v) Kuanzia mwaka 2010/2011, Halmashauri zinatakiwa kuonesha bakaa katika akaunti ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha ili zijumuishwe kwenye bajeti ya mwaka unaofuata kama chanzo cha mapato;

(vi) Katika Mwaka 2010/2011, Serikali itatumia utaratibu wa malipo unaosimamiwa na Benki Kuu *(Tanzania Interbank Settlement System - TISS)* kwa malipo yatakayofanywa na Wizara zote zilizopo Dar es salaam na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa

Dar es Salaam ili kuharakisha malipo ya Serikali. Hatua zimechukuliwa kulinda mfumo huo kutokana na athari zinazoweza kutokea;

(vii) Kudhibiti utoaji wa dhamana za Serikali kwa vyombo mbalimbali vya umma ili kuepuka ongezeko lisilohimilika la deni la Taifa; na

(viii) Serikali itakuwa na chombo maalum kitakachosimamia ujenzi na viwango vya majengo ya Serikali ili kuwa na majengo yatakayokidhi viwango *(standards)* vitakavyowekwa.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuendelea kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, Serikali imefanya marekebisho kadhaa kwenye Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 yatakayowasilishwa kwenye Bunge hili.

Marekebisho hayo yataiwezesha Hazina, kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, kusimamia matumizi ya Fedha za Umma katika ngazi ya Serikali za Mitaa.

Aidha, marekebisho hayo yatawezesha uanzishwaji wa Idara Kuu ya Ukaguzi wa Ndani kitaifa ili kuimarisha utendaji wa Wakaguzi wa Ndani katika Wizara, Idara na Halmashauri. Idara hii itawajibika moja kwa moja kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali, pamoja na kuwa na wataalamu wa ukaguzi wa ndani, itahusisha pia wataalamu wa ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit)* na Usimamizi wa Mali za Serikali, ili kuiwezesha Serikali kutimiza azma ya kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ukaguzi wa ndani kwa kutoa mafunzo, kufuatilia kwa karibu matumizi ya Serikali, kufanya uhakiki wa mishahara inayolipwa kwa watumishi wa Serikali na kuitumia kikamilifu Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali inayoundwa kusimamia na kudhibiti fedha za umma. Aidha, uimarishwaji wa mtandao wa kompyuta wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha *(IFMS)* katika ngazi zote za Serikali utaendelezwa ili kudhibiti matumizi na kuzuia malimbikizo ya madeni unaotokana na kutotumia mtandao huu. Pamoja na uimarishaji wa *IFMS,* Serikali itaanzisha *database* ya miradi itakayounganishwa na *IFMS* kwa urahisi wa kufuatilia fedha inayotolewa na kutumika katika miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maslahi ya watumishi. Serikali ya Awamu ya Nne inatambua umuhimu wa kuwa na maslahi bora ya wafanyakazi katika kuongeza ufanisi na tija. Serikali inachukua hatua za kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika mwaka 2010/2011. Sanjari na hatua hii, utaratibu wa kuhakiki mishahara utaendelea ili kudhibiti malipo kwa wafanyakazi hewa.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mashirika ya umma. Katika miaka ya hivi karibuni, pamejitokeza changamoto nyingi katika kusimamia mashirika na taasisi za umma. Baadhi ya mashirika na taasisi za umma zimeshindwa kujiendesha kwa ufanisi na

kuwa mzigo mkubwa kwa Serikali kwa kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu kinyume na lengo la kuanzisha mashirika na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuboresha usimamizi wa mashirika na taasisi za umma kwa lengo la kuongeza ufanisi, tija, mapato na kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Katika Mkutano wa 19 wa Bunge uliyofanyika mwezi Aprili, 2010, Serikali iliwasilisha na Bunge kupitisha marekebisho ya Sheria ya Mashirika ya Umma Sura 257 na Sheria iliyoanzisha Ofisi ya Msajili wa Hazina Sura 370. Marekebisho haya yanalenga kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kuwa mamlaka inayojitegemea kisheria yenye jukumu la kusimamia utendaji na ufanisi katika mashirika na taasisi za umma. Kufuatia marekebisho haya, muundo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina utapitiwa upya ili kuiwezesha ofisi hii kuwa na taaluma za kuwezesha kusimamia kwa karibu zaidi utendaji katika mashirika na taasisi za umma. Serikali itaendelea kufanya tathmini ya mashirika na taasisi zake ili kubaini changamoto zilizopo na kuzitafutia ufumbuzi kwa lengo la kuimarisha ufanisi katika kusimamia rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na hatua nyingine za mapato. Serikali itaendelea kupanua wigo wa kodi na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato ili kuweza kugharamia sehemu kubwa ya Bajeti. Aidha, Serikali itaendelea kurejea sheria na taratibu zinazosimamia misamaha ya kodi kwa nia ya kuipunguza na kudhibiti usimamizi wake. Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* itaendelea kutekeleza mpango wake wa tatu wa maboresho *(Third Corporate Plan)* wa miaka mitano (2008/2009 – 2012/2013) ambao ndio umekuwa chachu na msingi wa kukua kwa mapato ya ndani. Vile vile Serikali itaimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi ili yaweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, maboresho hayo yatahusu sheria zifuatazo:-

(a) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148;
(b) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
(c) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147;
(d) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290;
(e) Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari), Sura 124;
(f) Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168;
(g) Sheria ya Bodi ya Korosho, Sura 203;
(h) Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Tax)*, Sura 40;
(i) Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, ya mwaka 2004;
(j) Misamaha ya kodi ya Magari kupitia sheria za kodi na matangazo ya Serikali *(GNs);*
(k) Marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi;
(l) Marekebisho ya Ada na Tozo Mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea;

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148; kwa kuzingatia azma ya Serikali ya kutoa kipaumbele katika kukuza uzalishaji kwenye sekta za kilimo na mifugo na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148, kama ifuatavyo: -

(i) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye usafirishaji wa mazao ya kilimo kutoka shambani hadi kwenye viwanda vya usindikaji kwa wakulima wenye kilimo cha mkataba wa miwa, mkonge na chai;(*Makofi*)

(ii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirisha na kusindika maziwa ili kuhamasisha uwekezaji katika sekta ndogo ya maziwa na kuboresha kipato kwa wananchi. Mashine na Vifaa vitakavyohusika na msamaha huu ni kama ifuatavyo: -

(a) Vifaa maalum vya kubebea maziwa (*Milk cans – HS Code. 7310.29.90);*

(b) Pampu maalum za kusukuma maziwa (*Milk pumps- HS Code no. 8413.81.00*);

(c) Bomba maalum la kupitishia maziwa kwenye viwanda vya usindikaji - *Milk hoses (HS Code. no 8413.70.20);*

(d) Kompresa maalum zinazotumika kwenye vifaa vya kupoza maziwa (*Compressors used in refrigerating equipment - HS Code 8414.30.00);*

(e) Matanki ya kuhifadhia maziwa (*Storage tanks, - HS Code 7309.00.00);*

(f) Gari maalum lenye kifaa cha kupoza na kusafirisha maziwa *(HS Code 8716.31.90);*

(g) Mtambo maalum wa kuchemsha maziwa *(Milk pasteurizers - HS Code 8434.20.00);*

(h) Kifaa maalum cha kuchekecha maziwa ili kutoa siagi *(Butter churns -HS Code 8434.90.00);*

(i) Vifaa maalum vya kupoza na kutengeneza ubaridi *(HS Code 8415.81.00);*

(j) Kifaa maalum cha kukandamiza mabonge ya maziwa na kukamua maji ili kuzalisha jibini – *(Chees pressers, HS Code 8434.20.00). (Makofi)*

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha ufugaji bora na kuwawezesha wakulima wa mbegu za mafuta kupata bei yenye tija kwa mauzo ya bidhaa hiyo;

(iv) Kuvipa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani vifaa vinavyouzwa kwa wataalamu wa mifugo waliosajiliwa kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ili unafuu huu utolewe katika Jedwali la Tatu *(Special Relief Supplies)* badala ya Jedwali la Pili *(Exempt Supplies*) la sheria hiyo;

(v) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye zana za kilimo kama vile; kivuna nafaka *(combine harvester*), pick up balers, hay making machinery na *mowers* vinavyotumika mahsusi kwenye uzalishaji wa kilimo na mifugo;

(vi) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani katika usafirishaji wa maua kwa ndege kwenda nje ya nchi;

(vii) Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua *(green houses); (Makofi)*

(viii) Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji wa bidhaa na huduma zitolewazo kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya vyama vya ushirika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mashamba kama vile mitaro ya umwagiliaji, barabara za mashambani, ujenzi wa maghala au huduma nyinginezo za namna hiyo; na*(Makofi)*

(ix) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kuzalisha mifugo *(breeding services)* kwa njia ya kupandisha mifugo na kutumia mashine maalum za kuzalishia/kutotolea vifaranga (*incubators*); *(Makofi)*

(x) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha napenda kufanya marekebisho ya sheria hiyo ili kuhamasisha uwekezaji na uzalishaji katika sekta ya viwanda hapa nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa waendelezaji *(developers)* wa maeneo ya uwekezaji ya *EPZ/SEZ;*

(ii) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini; *(Makofi)*

(iii) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya juisi za matunda na bidhaa za maziwa. Hatua hii inalenga katika kupunguza gharama za uzalishaji na kuboresha thamani ya bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vya juisi na maziwa hapa nchini; na

(iv) Kurejesha utaratibu wa kutambua baadhi ya vifaa kama bidhaa za mtaji *(deemed capital goods)* kwa baadhi ya wawekezaji kwa nia ya kuvipa unafuu wa kodi. Hata hivyo, ili kudhibiti matumizi mabaya ya utaratibu huo yanayoweza kuvujisha mapato, Serikali itaunda Kamati maalum *(Inter disciplinary committee)* itakayosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ili kufuatilia na kuratibu mchakato wa utoaji wa unafuu pamoja na udhibiti wa matumizi yake. Aidha, itaandaliwa orodha ya bidhaa husika ili zijulikane waziwazi. *(Makofi)*

Hatua hizi katika Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.39.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332. Napendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

(i) Kurekebisha kifungu cha 11 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuweka wigo wa ukomo *(ring fencing)* wa maeneo ya uchimbaji wa madini kwa nia ya kudhibiti gharama zinazotakiwa kutolewa katika kukokotoa faida itakayotozwa kodi ya mapato kuwa ni zile za eneo husika tu. Hatua hii itahusisha kampuni zote za Madini;

(ii) Kupunguza kiwango cha chini cha Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 14 sambamba na nyongeza ya kima cha chini cha mshahara kitakachotangazwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma. Lengo ni kuwaongezea kipato na kuwapunguzia mzigo wa kodi watumishi wa umma wenye kipato cha chini; na

(iii) Kwa kuwa bado kuna biashara nyingi zinazofanywa na watu wasiokuwa na namba za utambulisho wa mlipa kodi *(TIN)*, napendekeza kodi ya zuio inayozuiwa na Serikali kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma wasiokuwa na *TIN* izuiwe pia na wafanyabiashara wote waliosajiliwa ili kuwahamasisha wasiokuwa na namba za utambulisho kwenda kusajiliwa. Hatua hizi za Kodi ya Mapato zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 4.468.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147. Napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura ya 147 kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo kutoka shilingi 97 hadi shilingi 80 ili kupunguza gharama za uzalishaji wa bidhaa hapa nchini; hatua hii imezingatia dhamira ya Serikali ya kukuza viwanda, ajira na mapato ya ndani. Aidha, punguzo hili limezingatia makubaliano ya Serikali na wenye viwanda ya kupunguza ushuru huo hadi kuufuta kabisa katika kipindi cha miaka mitatu.

(ii) Kurekebisha kwa asilimia 8 viwango maalum vya ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zinazotozwa ushuru huu isipokuwa zile za mafuta ya petroli. Marekebisho haya yanazingatia kiasi cha wastani wa mfumuko wa bei. Viwango vya sasa na vile vinavyopendekezwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Vinywaji baridi kutoka shilingi 58 kwa lita hadi shilingi 63 kwa lita;
(b) Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa, kutoka shilingi 209 kwa lita hadi shilingi 226 kwa lita;
(c) Bia nyingine zote, kutoka shilingi 354 kwa lita hadi shilingi 382 kwa lita;
(d) Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka shilingi 1,132 kwa lita hadi shilingi 1,223 kwa lita; na
(e) Vinywaji vikali, kutoka shingi 1,678 kwa lita hadi shilingi 1,812 kwa lita.

(iii) Kurekebisha viwango vya Ushuru wa bidhaa kwenye sigara kama ifuatavyo: -

(a) Sigara zisizo na kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75 kutoka shilingi 5,749 hadi shilingi 6,209 kwa sigara elfu moja;

(b) Sigara zenye kichungi na zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka shilingi13,564 hadi shilingi 14,649;

(c) Sigara nyingine zenye sifa tofauti na (a) na (b) kutoka shilingi 24,633 hadi shilingi 26,604 kwa sigara elfu moja;

(d) Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara *(cut filler)* kutoka shilingi 12,441 hadi shilingi 13,436 kwa kilo; na

(e) Ushuru wa (*Cigar*) unabaki asilimia 30.

Hatua hizi katika Ushuru wa Bidhaa kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 20.042.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290. Napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba wanazoishi wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 ambao hali zao za kiuchumi haziwawezeshi kulipa kodi hiyo. Hata hivyo, msamaha huu utatolewa kwa wale watakaothibitishwa na uongozi katika Serikali za Mitaa kuwa kweli hawana uwezo wa kulipa kodi husika; na

(ii) Kiwango cha kutoza ushuru wa mazao shambani kiwe kati ya asilimia 3 na asilimia 5 ya bei ya kuuza mazao shambani ili kuzipa fursa Halmashauri na Serikali za Mitaa kutoza ushuru huo kulingana na uwezo na raslimali walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari), Sura 124. Napendekeza kufanya marekebisho ya Ada ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari (Magari na Pikipiki) kama ifuatavyo: -

(i) Ada ya kusajili gari kutoka shilingi 120,000 za sasa hadi shilingi 150,000; na

(ii) Ada ya kusajili pikipiki kutoka shilingi 35,000 za sasa hadi shilingi 45,000.

Hatua hizi katika kuongeza viwango vya Ada za Magari na Pikipiki kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi 3.19 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168. Napendekeza kufanya marekebisho yafuatayo katika Ada ya mwaka ya leseni za Magari *(Annual Motor Vehicle Licence Fee): -*

(i) Gari lenye Ujazo wa Injini 0-500.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 30,000 hadi shilingi 50,000;

(ii) Gari lenye Ujazo wa Injini 501-1500.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000;

(iii) Gari lenye Ujazo wa Injini 1501-2500.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000; na

(iv) Gari lenye Ujazo wa Injini zaidi ya 2501.cc kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 150,000 hadi shilingi 200,000.

Hatua hizi katika kuongeza viwango vya ada ya mwaka ya leseni za magari kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 16.981.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Bodi ya Korosho – Sura 203. Napendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa kusafirisha nje korosho ghafi kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15 au dola za Kimarekani 160 kwa tani moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo ni kulinda viwanda, kuongeza ubora na thamani ya korosho na kukuza ajira kwa wananchi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.613. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ya kodi ya michezo ya kubahatisha *(Gaming Tax)*, Sura 40. Napendekeza kuongeza kiwango cha kodi inayotozwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha kutoka shilingi 16,000 kwenda shilingi 32,000 na kutoza kodi ya kiwango cha asilimia 13 ya mapato kwenye Mashine ya Tombola *(Sloating machine).* Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 0.5.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004: Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya kikao cha maandalizi ya Bajeti tarehe 12 Mei, 2010, Kampala, Uganda na kujadili mapendekezo ya

marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Forodha kwa mwaka 2010/2011 yaliyowasilishwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (Tanzania, Kenya, Uganda na Rwanda).

Aidha, Mawaziri wa Fedha walipitia viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha *(Common External Tariff)* kulingana na matakwa ya Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayoelekeza kwamba nchi wanachama zipitie viwango hivyo baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo yao, Mawaziri wa Fedha wamezingatia kuwepo na soko la pamoja katika Jumuiya na hivyo walikubaliana kuboresha sekta za viwanda, kilimo na usafirishaji kama vichocheo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika sekta ya viwanda walikubaliana kufanya marekebisho yafuatayo:-

(i) Kuongeza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwenye vipitishi joto au umeme vya aluminiamu iliyowazi na nyaya *(bare aluminium conductors and cables)* za *HS Code No. 7614.10.00* na *7614.90.00* kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 25 kwa lengo la kuvilinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo katika nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki dhidi ya ushindani usio wa haki kutoka nje.

(ii) Kuongeza kiwango cha Ushuru wa Forodha kwa nyaya za umeme *(HS Code 7413.00.90)* kutoka asilimia 10 hadi asilimia 25 ili kuwianisha na Ushuru wa Forodha unaotozwa kwa shaba nyekundu *(Copper wire)* ambayo ni bidhaa shindani na inatozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25.

(iii) Kuondoa Ushuru wa Forodha unaotozwa kwenye malighafi ambazo hutumika katika uzalishaji wa bidhaa zenye msamaha. Hatua hii inalenga katika kuweka mazingira mazuri ya kiushindani kwa kuwa baadhi ya malighafi hizo hutozwa ushuru wa asilimia 10 au asilimia 25. Aidha, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zitatakiwa kuwasilisha orodha ya malighafi hizo kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya utekelezaji. Kwa kuzingatia makubaliano hayo, wenye viwanda hapa nchini wanatakiwa kupeleka orodha ya malighafi husika Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ili hatimaye iweze kuwasilishwa kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0) kwa malighafi ya viwanda vya kutengeneza rangi *(driers)* inayotambuliwa chini ya *(HS Code 3211.00.00)*.

(v) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0) kwa malighafi za viwanda vya saruji *(Petroleum coke, not calcined)* inayotambuliwa chini ya *(HS Code 2713.11.00)*.

(vi) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0) kwenye malighafi zinazotumika kutengeneza kadi zinazotumiwa

na makampuni ya simu kuuza muda wa maongezi *(Stamping foils) (HS Code 3212.10.00).*

(vii) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia sifuri (0) malighafi ya viwanda vya kutengeneza rangi inayotambuliwa chini ya *(HS Code 3212.90.10).*

(viii) Kusamehe Ushuru wa forodha kwa kutumia utaratibu wa *duty remission scheme* malighafi za kutengeneza majalada ya vitabu *(textile garments coated with gum) (HS Code 5901.10.00).*

(ix) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwa kutumia utaratibu wa *duty remission scheme* kwa malighafi za viwanda vya kutengeneza viatu *(Looped pile fabrics of manmade fibres) HS Code 6001.22.00.*

(x) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia sifuri (0) malighafi za viwanda vya vyuma *(HS Code 7210.11.00).*

(xi) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kwenye malighafi za viwanda vya vyuma. *(HS Code 7212.10.00);* na

(xii) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwenye ngano inayotambulika chini ya *(HS Code 1001.90.20)* na *(HS Code 1001.90.90)* kwa muda wa mwaka mmoja kwa vile bado uzalishaji wa bidhaa hiyo katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki haujaweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wamefanya maamuzi yenye kuboresha sekta ya usafirishaji ili iweze kuchangia zaidi katika kupunguza gharama za usafirishaji na kukuza uchumi. Ili kutekeleza azma hiyo, wamekubaliana kufanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea na msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa magari yenye uwezo wa kubeba tani 5 lakini yasiyozidi tani 20 kama vile Fuso, Isuzu na mengineyo ya aina hiyo *(HS Code 8704.22.00)* na hivyo kutoza ushuru wa asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(ii) Kuendelea na msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye magari yenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 20 *(HS Code 8704.23.90)* na hivyo kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri (0) badala ya asilimia 25.

(iii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwa mabasi yatakayoingizwa nchini Tanzania kwenye mradi wa mabasi ya kwenda kasi *(Fast Truck Bus Project).* Hatua hii inalenga katika kuondoa adha ya usafiri inayosababishwa na msongamano wa magari ambao unaathiri shughuli za maendeleo (uzalishaji na biashara). Aidha, Serikali inaendelea na

ukarabati na upanuzi wa barabara na miundombinu ili kuwezesha mradi huo kuanza mapema iwezekanavyo.

(iv) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwa waunganishaji wa magari *(Motor Vehicles Assemblers)*; na

(v) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwa Matrekta ya kukokota matrela yanayotambulika chini ya *(HS Code 8701.20.90)*.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua za kuboresha kilimo na sekta nyinginezo zimehusisha marekebisho ya sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na viwango vya Ushuru wa Forodha kama ifuatavyo:-

(i) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye taa/balbu zinazotengenezwa kwa kutumia teknolojia ya *Emitting Diodes (LED)* kwa lengo la kuhamasisha matumizi madogo ya umeme.

(ii) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwenye kuku wazazi *(parent stock) (HS Code 0105.99.00)* kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya ufugaji wa kuku. Aidha, hatua hii inalenga katika kuhamasisha uagizaji kuku wazazi kutoka nje kwa lengo la kukuza uzalishaji wa kuku wa nyama na mayai hapa nchini.

(iii) Kuendelea na utaratibu wa kutotoza Ushuru wa Forodha bidhaa zinazouzwa kwenye Migahawa ya Majeshi ya Ulinzi na Usalama *(Armed Forces Canteen)* kwa mwaka mmoja.

(iv) Kurekebisha kifungu kinachosamehe Ushuru wa Forodha wa magari kwenye Jedwali la 5 la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa wananchi wanaorejea nchini *(returning resident)* ili kuweka kipindi cha miaka minne kabla mwombaji hajapata msamaha mwingine wa namna hiyo. Hatua hii inalenga katika kudhibiti matumizi mabaya ya msamaha huu.

(v) Kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 *(HS Code 2523.29.00)* kwenye Saruji kwa muda wa mwaka mmoja. Aidha, stadi itafanywa ili kujua viwango vya uzalishaji, mahitaji na bei ya saruji katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo itawawezesha Mawaziri wa Fedha kufanya uamuzi sahihi wa kiwango cha Ushuru wa Forodha kwa bidhaa hiyo.

(vi) Kuendelea kutoza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha cha asilimia 35 au dola za Kimarekani 0.20 *(U$ 0.20)* kwa kilo kwa nguo za mitumba *(HS Code 6309.00.00)*. Aidha, nchi wanachama zimekubaliana kupiga marufuku uingizaji wa nguo za ndani *(under garments)*.

(v) Kupunguza kiwango cha Ushuru wa Pamoja wa Forodha kwa Majiko yanayotumia gesi kutoka asilimia 25 hadi asimilia 10 *(HS Code 7321.11.00)*; na

(vi) Kusamehe Ushuru wa Forodha kwa glavu *(examination gloves) HS Code 4015.19.00* zinazotumika katika hospitali na maabara.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi katika Ushuru wa Forodha na marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha kwa pamoja zitapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni 4.175.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi ya magari kupitia sheria za kodi na matangazo ya Serikali *(GNs);* napendekeza kufanya marekebisho kwenye sheria husika za kodi na matangazo ya Serikali yanayotoa msamaha wa magari kwa walengwa mbalimbali ili kuweka ukomo wa umri wa miaka kumi kwa magari hayo. Lengo la hatua hii ni kupunguza wimbi la uagizaji wa magari chakavu na kuhifadhi/kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi; napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika Sheria mbalimbali za kodi ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya ada na tozo mbalimbali za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, tarehe ya kuanza kutekeleza hatua mpya za kodi, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 01 Julai, 2010, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa Bajeti kwa mwaka 2010/2011, kwa kuzingatia sera za uchumi jumla pamoja na misingi na sera za Bajeti, Serikali inatarajia kukusanya mapato ya ndani ya jumla ya shilingi bilioni 6,003.590 (trilioni 6.0) katika kipindi cha mwaka 2010/2011. Kiwango hiki cha mapato ni sawa na asilimia 17.3 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 16.4 mwaka 2009/2010. Mapato kutokana na vyanzo vya Halmashauri yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 172.582 na mapato kutokana na ubinafsishaji shilingi bilioni 30.0.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 11,609.557 (trilioni 11.6) katika mwaka 2010/2011 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Matumizi haya yatagharamiwa na mapato ya ndani, mikopo ya ndani na nje, pamoja na misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuendelea kuisaidia Bajeti yetu mwaka 2010/2011 kwa kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,274.553 (trilioni 3.27). Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 821.645 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 2,452.91 (trilioni 2.4) ni misaada na mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kukopa kiasi cha shilingi bilioni 2,128.832 (trilioni 2.1) kutoka vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 797.62 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva *(roll-over)* na shilingi bilioni 1,331.2 (trilioni 1.3) ni mikopo mingine itakayotumika kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Bajeti umezingatia kwa makini matokeo ya hatua za kodi nilizozifafanua hapo awali. Hivyo, jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa sura ya Bajeti kwa mwaka 2010/2011.

**SURA YA BAJETI MWAKA 2010/2011**

| | **Mapato** | **Shilingi Milioni** | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **A.** | Mapato ya Ndani | 6,003,590 | | | |
| | (i) Mapato ya Kodi (TRA) | | 5,652,590 | | |
| | (ii) Mapato yasiyo ya Kodi | | 351,000 | | |
| **B.** | Mapato ya Halmashauri | | | 172,582 | |
| **C.** | Misaada na Mikopo ya Kibajeti | | | 821,645 | |
| **D.** | Misaada na Mikopo ya Miradi ya Maendeleo na ya Kisekta | | 2,452,908 | | |
| | (i) Misaada na Mikopo ya Miradi | | | 1,975,120 | |
| | (ii) Misaada na Mikopo ya Kisekta | | | 477,788 | |
| **E.** | Mikopo ya Ndani na Nje | | 1,331,212 | | |
| **F.** | Mikopo kulipia dhamana na hatifungani za Serikali zilizoiva *(Roll-over)* | | | | 797,620 |
| **G.** | Mapato kutokana na Ubinafsishaji | | | | 30,000 |
| **JUMLA YA MAPATO YOTE** | | | | | **11,609,557** |

Matumizi

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **H.** | Matumizi ya Kawaida | 7,790,506 | | |
| | (i) Deni la Taifa | 1,756,044 | | |
| | (ii) Wizara | | 4,155,768 | |
| | (iii) Mikoa | | 119,580 | |
| | (iv) Halmashauri | 1,759,114 | | |
| **I.** | Matumizi ya Maendeleo | 3,819,051 | | |
| | (i) Fedha za Ndani | | 1,366,143 | |

| | |
|---|---|
| (ii) Fedha za Nje | 2,452,908 |
| **JUMLA YA MATUMIZI YOTE** | **11,609,557** |

Mheshimiwa Spika, naomba kufanya marekebisho kidogo katika Ukurasa wa 55 mwisho wa aya ya 53, tutaongeza haya:-

Kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za petroli kwa kampuni za madini zilizosaini mikataba na Serikali. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika mikataba kati ya Serikali na makampuni yaliyosaini mikataba kabla ya tarehe 1 Julai, 2009.

Ukurasa wa 55, mwisho wa aya namba 63 tunafanya marekebisho: Kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa za petroli kwa kampuni za madini zilizosaini mikataba na Serikali *(Mineral Development Agreement)*. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika mikataba kati ya Serikali na makampuni ya madini yaliyosaini mikataba kabla ya 1 Julai, 2009. Tumeelewana? Eeh!

*(Hapa kelele zilisikika kutoka kwa Wabunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusipate taabu sana! Namwelekeza Katibu kwamba badiliko hili ambalo litakuwapo katika *Hansard*, mtagawiwa kesho asubuhi, mtakuwa nalo! Ahsante! *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ninataka kuliweka (samahani nilisahau wakati nasoma), *page 53* mwisho wa aya ya namba 60, kifungu namba 9. Kutoa unafuu maalum wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kampuni za madini zenye mikataba na Serikali. Aidha, msamaha huu utatolewa kwa mujibu wa masharti yaliyopo katika mikataba kati ya Serikali na makampuni ya madini yaliyosaini mikataba kabla ya 01 Julai, 2009. Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nitaziwasilisha hizi kwa Katibu wa Bunge ili ziweze kugawiwa na ziweze kuingia kwenye *Hansard (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Bajeti ya mwaka 2010/2011 ni mwendelezo wa jitihada za Serikali katika kufikia malengo ya MKUKUTA, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na hatimaye Dira ya Maendeleo 2025. Hata hivyo, ili kufikia malengo yetu mapema zaidi, kila mwananchi anapaswa kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zinazojitokeza kwa kuzalisha mali na kujiongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushiriki katika uzalishaji kwa wananchi mmoja mmoja au katika vikundi ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wetu. Aidha, sekta za kilimo, mifugo na viwanda zikiboreshwa na kutilia mkazo usindikaji wa mazao ya kilimo, zina nafasi kubwa ya kuchangia Pato la Taifa na kukuza ajira. Bajeti hii pia inalenga kuongeza jitihada za Serikali za kuendeleza ardhi na kuunganisha nchi yetu kwa njia ya miundombinu ya barabara, reli, mawasiliano na nishati.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapo awali, huu ni mkutano wa mwisho wa Bajeti kwa Bunge hili baada ya miaka mitano ya kwanza ya Serikali ya Awamu ya Nne. Wengi wetu kama nilivyosema awali, tutarudi kwa wananchi kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi yetu, kuomba ridhaa yao ya kurudi tena katika ukumbi huu. Nina matumaini makubwa kuwa wananchi hawatasahau kazi kubwa na nzuri iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Awamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na kwa kunipa heshima ya kuwa Waziri wa Fedha na Uchumi kwa nusu ya pili ya kipindi cha kwanza cha Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais kwa uongozi wake na hasa katika kutatua kero za Muungano. Vile vile, namshukuru Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge na Waziri Mkuu kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali Bungeni na kwa ushirikiano na maelekezo mbalimbali yaliyonisaidia kutekeleza kazi zangu kwa ufanisi. *(Makofi)*

Namshukuru Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendesha Bunge letu kwa viwango vya hali ya juu wakati wote. *(Makofi)*

Nawashukuru Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa wakati wa kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Fedha na Uchumi na mwisho, nachukua fursa hii kuwashukuru wapigakura wangu wa jimbo la Kilosa walionipa nafasi ya kuwa Mbunge wao kwa kipindi chote cha miaka mitano, ninaamini kwamba sikuwaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho kabisa napenda kumshukuru kwa dhati kabisa mke wangu Khalda, kwa uvumilivu kwa sababu miaka mitano haikuwa rahisi na wakati mwingi sikuwa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wanangu watano na wajukuu zangu sita kwa uvumilivu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina hakika itakuwa ni halali kabisa kwa niaba yenu nimshukuru Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo kwa hotuba hii aliyoisoma, si kazi rahisi katika mazingira haya kufanya ubunifu wa kutosha ili tuweze kuendesha nchi kwa kipindi

kingine cha miezi 12 ijayo. Lakini nadhani wamejitahidi kwa hiyo, kwa niaba yenu ninampongeza sana Mheshimiwa Mkulo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yanayofuta sasa yanatawaliwa na Kanuni ya 97 (1) na (2) lakini kwa kuwa tumetengua Kanuni sasa utaratibu wa kuzingatia hoja hii utakuwa kama ifuatavyo:-

Kwanza hoja hii itachangiwa kwa siku tatu siyo tano, pili, kwa maana hiyo basi uchangiaji utakuwa ni wa dakika kumi na siyo kumi na tano na hatimaye siku ya Jumatatu tarehe 14 Juni, 2010 atakapo hitimisha hoja Mheshimiwa mtoa hoja Waziri wa Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Kamati atapewa dakika zisizodi 30 ingeweza ikawa 40 kwa sababu wanachangia hotuba mbili ya asubuhi na hii lakini imetubidi tukubaliane iwe ni dakika 30 tu, ahaa ni kesho kweli ni kesho asubuhi samahani. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani naye anapewa dakika hizo hizo 30 na baada ya hapo mjadala utaendelea kwa siku ya kesho Ijumaa na siku ya kesho kutwa Jumamosi hadi usiku halafu ndiyo Jumatatu kuhitimisha na tayari nimepata orodha ya wachangiaji ambayo mtaikuta katika maeneo ya matangazo tayari wako 36 nilikwishapata 21 lakini wameongezeka tena 15 tutajitahidi nadhani kwa dakika 10 watu watalenga vipaumbele na bila kurudia rudia nadhani mjadala utakuwa mzuri tu kwa hiyo, ahueni tunayoipata ni kwamba hatuendelei na mjadala leo kwa hiyo, mna nafasi ya saa kadhaa ya kuweza kusoma vizuri hotuba. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninavyofahamu *Hansard* walivyo mahiri itakuwa vizuri Katibu tupate yale marekebisho mawili ili wale Wabunge ambao wanaweza kupita hapa au kwa namna yoyote ndani ya muda wa saa moja hivi wataweza kupata yale marekebisho yanayohusu ukurasa wa 53 na ukurasa wa 65 nadhani ili sasa iwe na picha kamili ya yaliyosomwa hapa.

Sina matangazo hapa na kwa hiyo, kwa shughuli za leo tumefikia mwisho na nina ahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 11.47 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 11 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*